epaper.ippmedia.com
www.ippmedia.com
0745 700710
LIKE & FOLLOW US
Alhamisi Juni 27, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • Na. 0581720
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
nipasheTZ nipasheTZ The Nipashe Digital nipasheTZ nipashedigital



UKURASA 22
**DESCHAMPS: MASKI 'INAMKERA' MBAPPE**

## SAKATA LA SUKARI

# Wakala Chakula wapewa jukumu

• **Siri** upandaji holela wa bei, hujuma za waagizaji wakubwa... *Endelea ukurasa 2*





Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Mipango, Uwekezaji, Prof Kitila Mkumbo

Waziri wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba

UKURASA WA 2

### MBOWE: MIAKA SABA WATANZANIA WANALALAMIKA KILA KONA NCHINI

MWENYEKITI wa Taifa wa Chama cha Demokrasia na...



UKURASA WA 5

### SERIKALI YAIPATIA DAWA ZA MILIONI 100/- KLINIKI YA MAKONDA ARUSHA

SERIKALI imetoa dawa zenye thamani ya zaidi Sh. milioni...



UKURASA WA 19

### RUTO AAHIRISHA KUHALALISHA MUSWADA, RAIA WAKE UINGEREZA NAO WAMGOMEA

RAIS wa Kenya, William Ruto, amekataa kutia saini muswada wa fedha wa...

## Mgomo wa wafanyabiashara wasambaa hadi kusini, nyanda za juu

UKURASA 3



## Serikali: Nyongeza ya asilimia 7 kikokotoo si haba, isibezwe

UKURASA 2

**MICHEZO** **SERIKALI: YANGA, SIMBA SAJILINI KIMATAIFA** UK.24 **KATUNI** UK.6

# Wakala Chakula wapewa jukumu sukari

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Fedha, Dk. Mwigulu Nchemba, amesema serikali itaanza kuutumia Wakala wa Hifadhi ya Chakula (NFRA), kununua na kuhifadhi sukari ili kumaliza shida ya sukari ambayo imekuwa ikijitokeza mara kwa mara nchini.

Dk. Nchemba alisema hayo jana Bungeni wakati akijibu hoja zilizotolewa na wabunge wakati wa kuhitimisha mjadala wa bajeti ya serikali kwa mwaka wa fedha 2024/25.

Alisema NFRA, inakwenda kutibu shida ya kupanda mara kwa mara kwa bei ya sukari nchini hali ambayo imekuwa ikiibua maswali na malalamiko kutoka kwa wananchi.

"Tunakwenda kuanza kuitumia NFRA kununua sukari na kuhifadhi kama ambavyo imesaidia katika kuhifadhi mazao mengine ya chakula," alisema Dk. Mwigulu.

Aidha, alisema NFRA inatumika kutokana na kufanya vizuri katika kuhifadhi mazao mengine kwa ajili ya usalama wa chakula.

"Kesho nitasoma muswada wa sheria ya fedha ambao hapa bungeni utakwenda kuruhusu kutumika kwa NFRA kununua na kuhifadhi sukari kuanzia mwaka mpya wa fedha na hii itakwenda kutibu upandaji wa bei ya sukari holela," alisema.

Alisema, serikali hutoa msamaha wa kodi na tozo katika bidhaa mbalimbali nchini, lakini hali hiyo imekuwa haiwanufaishi wananchi wa kawaida na badala yake wameitumia fursa hiyo kwa maslahi yao binafsi.

"Tumetoa msamaha kwenye taulo za kike hakuna kilicho badilika, tumetoa ruzuku ya mafuta wananchi hawajanufaika chochote wafanyabiashara wamechukua hii kama fursa kwao kujinufaisha wenyewe kwa maslahi yao binafsi hivyo tunakwenda kuanza kutumia NFRA kununua na kuhifadhi sukari kama ambavyo tumefanya katika mazao mengine ili kutibu tatizo la sukari," alisema.

Aidha, alisema moja ya hoja iliyoibuliwa na wabunge wakati wa kuchangia mjadala wa bajeti kuu ni suala la malipo ya makandarasi.

Kuhusu malalamiko ya wafanyabiashara mambo mbalimbali ambayo yamekuwa kero kwao, Dk. Mwigulu alisema hakuna haja ya kugoma kwa kuwa serikali ya awamu ya sita ni sikivu na kila walicho kilalamikia kitafanyiwa kazi.


"Hatuna sababu ya kufika huko tunarudishana nyuma, serikali hii sikivu imesikia kilio cha wafanyabiashara na kila hoja yao itafanyiwa kazi kama ambavyo mambo mengine tumeyashughulikia," alisema.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo, alisema serikali inaendelea na jitihada za kuongeza uzalishaji wa bidhaa zinazotumika kwa wingi nchini ili kupunguza uagizaji kutoa nje ya nchi.

"Bidhaa hizi ni pamoja na mafuta ya kula, ngano mazao ya chakula, dawa mavazi na kadhalika pia tunaendelea kulinda uwekezaji unaochochea uwekezaji nchini," alisema.

Alisema lengo la serikali ni kujitosheleza kwa sukari na kuondokana na shida ya 'Gap Sugar' kwa kuwekeza katika sekta ya kilimo ili kuongeza uzalishaji wa mazao ambayo yatatumiwa na viwanda vya ndani kuzalisha bidhaa hiyo.

"Tuachane watu ambao wanasema serikali ina nia ya kuua viwanda vya ndai vya sukari kama tungekuwa tunataka kuua basi tusinge samehe kodi ya Sh. bilioni 240 kwa viwanda vya ndani vinavyozalisha sukari ili kuvijengea uwezo," alisema Prof. Mkumbo.



Rais Samia Suluhu Hassan akisalimiana na Mnadhimu Mkuu wa Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Luteni Jenerali Salim Haji Othman (wa tatu kulia) pamoja na Mkuu wa Utumishi Jeshini, Meja Jenerali Marco Gaguti (wa pili kulia), baada ya kuwasili katika Chuo cha Taifa cha Ulinzi (NDC), Kunduchi jijini Dar es Salaam jana. Rais Samia, alitoa mada ya falsafa ya R-Nne (4Rs), ambazo ni Maridhiano, Ustahimilivu, Mageuzi na Kujenga upya, ambayo anaitumia katika kuongoza Serikali ya Awamu ya Sita, katika mhadhara chuoni hapo. **PICHA: IKULU**

# Mbowe: Miaka 7 kila kona malalamiko

**Na Godfrey Mushi,** MBULU

MWENYEKITI wa Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, amesema Tanzania ni nchi pekee isiyo na vita, lakini wananchi wake wakati wote wanalalamika.

Amesema miaka saba iliyopita ni miongoni mwa nchi za mwisho tano zisizo na furaha.

Jana, akiwa Kata ya Dongobesh, Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu, mkoani Manyara katika mwendelezo wa mikutano yake ya kampeni mikoa ya Kanda ya Kaskazini, Mbowe alisema wanajiuliza nchi haina vita, lakini hizo nchi nyingine ambazo hazina furaha, zina vita.

"Tujadili maisha yetu, tumetoka wapi, tuko wapi na tunapaswa kwenda wapi. Ni jambo la bahati mbaya sana, karibu kila mahali wanalalamika, kila unapokwenda watumishi wanalalamika, kila unapokwenda wanafunzi wanalalamika.

"Kila unapokwenda nchi hii wafugaji wanalalamika. Kila mahali kuna kilio, wanalalamika. Tunajiuliza kwa nini Watanzania hawana furaha. Umoja wa Mataifa wanafanya survey ambayo inaitwa World Happiness Index, yaani unapima mataifa na raha ya kila taifa.

Tanzania ndio nchi pekee isiyo na vita, lakini wananchi wake wakati wote wanalalamika. Wananchi wanalalamika kwa sababu mbalimbali."

Mbunge wa zamani wa Arusha na Mwenyekiti wa CHADEMA, Kanda ya Kaskazini, Godbless Lema alisema:

"Leo tunafanya mikutano mitano. Nilikuwa natafuta hizi data (takwimu), Tanzania wananunua maziwa kila mwaka bilioni 34.5 kutoka nje ya nchi.

"Nyie mkipewa ng'ombe wanaozalisha maziwa kwa wingi, mkatengenezewa mashamba ya kuzalisha vyakula vya ng'ombe, hamuwezi kufuga ng'ombe nyie?"

"Mahindi pamoja na kulima wanaleta ya bilioni 64, sukari bilioni 265, mchele tunanunua kila mwaka bilioni 146, maharage ya soya bilioni 34, njano bilioni 554 na mafuta ya kula bilioni 694. Jumla yake karibu trilioni mbili.

Vyakula vyote hivi, bidhaa zote hizi zinaweza kulimwa Mkoa wa Manyara peke yake. Yaani maana yake trilioni mbili ikibaki Manyara kila mwaka kwenye mazao huku tusingeona lami za kubabaisha, kungekuwa na lami, kungekuwa na vyuo, watoto wangesoma na watu wangekuwa na maisha bora.

Uchumi ni maarifa, ndio sababu Abu Dhabi (Makao Makuu ya Falme za Kiarabu-UAE), ni jangwa, lakini wana uchumi mzuri kuliko Tanzania.

"Hanang' kuna shamba la ngano, yale mashamba yamekufa. Leo tunaagiza ngano ya bilioni 500 Ukraine. Jiulize bilioni 500 ingekuwa inabaki Hanang' kila mwaka Hanang' ingekuwa kubwa kuliko Dar es Salaam. Kahawa, Mwenyekiti (Mbowe) anajua zaidi kuhusu kahawa."

# ...Serikali: Nyongeza ya 7% kwenye kikokotoo isibezwe

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Fedha, Ahmad Chande, amesema nyongeza ya asilimia saba kwenye kikokotoo cha mafao ya wastaafu ni kitu kikubwa kisichopaswa kubezwa.

Chande aliyasema hayo jana bungeni wakati akichangia mjadala wa mapendekezo ya bajeti ya serikali kwa mwaka ujao wa fedha.

"Kutoka asilimia 33 hadi 40 ni kikubwa sana na Mheshimiwa Spika, hata kama ingekuwa asilimia moja tu ingekuwa ni hatua kubwa sana kwa sababu wahenga wanasema 'jicho hutaraji haja kila namna na penye moja na moja si moja tena'. Kwa hiyo, hata ingekuwa moja ingetosha," alisema.

Chande alisema wafanyakazi wengi wameshukuru na baadhi ya wabunge wametoa shukrani kuhusu jambo hilo, akisisitiza "asiyeshukuru kwa yai, basi na jogoo hachinjiwi".

Naibu Waziri huyo pia alisema watafanyia kazi ushauri ulitolewa na Kamati ya Bajeti kuhusu mikopo ambayo inakopwa na serikali ielekezwe kwenye miradi ya uzalishaji.



HABARI KITAIFA

# Mgomo wa wafanyabiashara wasambaa

**Na Waandishi Wetu**

BAADHI ya wafanyabiashara wenye maduka katika mikoa minne wameungana na wenzao wa Soko la Kimataifa Kariakoo kufunga biashara zao, huku mkoani Arusha wakitumia muda huo kucheza mpira wa miguu.

Mikoa mingine ambayo baadhi ya wafanyabiashara wake walifunga maduka jana ni Njombe, Mtwara na Songwe, huku baadhi ya wafanyabiashara katika Soko la Kimataifa Kariakoo pamoja na wa mikoa ya Mbeya na Mwanza wakiendelea na mgomo huo.

Jana Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alikutana na viongozi wa wafanyabiashara katika kikao cha ndani jijini Dodoma, kikitanguliwa na kile kilichofanyika mwanzoni mwa wiki hii kikihusisha viongozi wao na serikali.

Jumatatu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo, alitoa maazimio, ikiwamo kusitisha ukaguzi wa risiti za Kielekroniki (EFD) na ritani za kodi uliokuwa unafanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kupitia Mkoa wa Kikodi Kariakoo.

**WACHEZA MPIRA**

Jijini Arusha, wafanyabiashara walifunga maduka yao kwa zaidi ya saa sita jana na kutumia muda huo kucheza mpira na baadaye baadhi yao walifungua.

Christopher Jengele, mmoja wa wafanyabiashara hao alisema kuwa badala ya kushika mawe kuanza kupiga watu na kuwaumiza, wameona ni bora kucheza mpira ili kujenga afya wakisubiri viongozi wao kutoa kauli ya ama kufungua maduka au kuendelea na mgomo.

Alisema wamefunga maduka kwa kuwa wanaumia; wanalipa kodi ya chumba cha biashara Sh. milioni tatu kwa mwezi, ilhali machinga wanauza mbele ya maduka yao na hawatozwi kodi yoyote. Frank Laizer, mfanyabiashara mwingine jijini, alisema wamefunga maduka yao kuunga mkono wenzao waliotangulia kufanya hivyo kutokana na utiriri wa kodi unaowaumiza.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Mkoa wa Arusha, Kirenga Sway, alisema hawatambui mgomo huo na kuagiza wafanyabiashara wafungue maduka yao.

Katibu wa Wafanyabiashara Mkoa wa Arusha, Ahmednoor Jamal, alisema wafanyabiashara wasubiri tamko kutoka kwa viongozi wao wa kitaifa ili kujua serikali imekubali mambo mangapi kati ya hoja 28 walizowasilisha.

Mnunuzi wa bidhaa, Eliah Mteshibe, alisema serikali na wafanyabiashara hao wanapaswa kumaliza changamoto zao ili kutoa fursa kwao kununua bidhaa na kupeleka vijijini kuuza.

Wakati hali ikiwa hivyo jijini Arusha, wafanyabiashara katika Soko Kuu la Mtwara wametaja sababu ya kufunga maduka kuwa ni kutokana na viwango vya kodi walivyokuwa wakilipa awali kuongezeka katika mabanda yao ya biashara.

Issa Bakari, mfanyabiashara mkoani Mtwara, alisema kumekuwa na ongezeko la kodi katika mabanda, linalotishia uhai wa biashara zao. Mkoani Mbeya, mgomo huo umeingia siku ya tatu. Masoko ya Mwanjelwa, Sido, Kabwe na Sokoine jana kulishuhudiwa shughuli kusimama na kuonekana watu wachache wakiwamo walinzi.

Mama lishe, Asha Mwakibinga, anayefanya shughuli zake katika soko la Mwanjelwa, alisema amepunguza kipimo cha chakula kutokana na uhaba wa wateja.

Mkoani Dar es Salaam, Mwenyekiti wa Wafanyabiashara Kariakoo, Martin Mbwana, alisema walizungumza na wafanyabiashara jana asubuhi kuwaeleza walichoteta na serikali na kuendelea kuwaomba wafungue maduka yao.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Said Mtanda, alisema jana kuwa wafanyabiashara watakaoona inafaa kufungua biashara zao wakati serikali ikiendelea kushughulikia changamoto zilizojitokeza, wafanye hivyo na wanaoona haifai waendelee kugoma.

"Tumewaita (wafanyabiashara) mmekataa kuja, sasa tutapataje suluhisho? Mnatakiwa kujenga utamaduni wa kukutana na kufanya mazungumzo pindi kunapotokea kutokuelewana.

"Mimi na menejimeti ya mkoa tupo,TRA, TANESCO, Mkurugenzi wa Jiji na wataalamu wanaohusika kukusanya kodi wapo hapa, tungejadiliana, lakini walalamikaji hawapo, tunawasaidiaje?" Mtanda alihoji.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyabiashara Tanzania wa Mkoa wa Mwanza, Patrick Masagati, alisema hakuna kiongozi yeyote wa jumuiya hiyo aliyehudhuria kikao hicho kwa kuwa barua ya wito wa kikao hicho walipata usiku.

Mfanyabiashara Soko la Makambako mkoani Njombe, Atukuzwe Ilomo, alisema licha ya serikali mwaka uliopita kukusanya maoni yao, kero bado ni nyingi, ikiwamo utozwaji Sh. milioni 15 wanapokutwa hawajatoa risiti.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wafanyabiashara mkoani humo, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini, Siphael Msigala, alisema serikali inapaswa kuweka kodi katika makundi mawili ili kuondoa mrundikano kwao.

**FREEMAN MBOWE**

Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), jana akizungumza na wananchi wa Kata ya Dongobesh, Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu, mkoani Manyara alisema hawapaswi kumtoza kodi mtu ambaye hawajui kipato chake.

"Mmesikia leo, tangu juzi wafanyabiashara wamegoma Dar es Salaam, si mmesikia? Wafanyabiashara wakubwa wanaosambaza bidhaa mbalimbali nchi nzima na wanaoagiza nje wamegoma.

"Wamegoma, wanasema 'biashara imekuwa kero, tunateswa na maofisa wa TRA, mitaji yetu inafilisika kwa ajili ya kodi. Tukigeuka kodi, tukigeuka faini'. Mtu anakuambia ana biashara ya mtaji wa milioni tano, anapigwa faini milioni 15," alisema.

Katika Mji wa Tunduma, mkoani Songwe zaidi ya maduka 500 katika Soko la Manzese na Soko Kuu la Halmashauri ya Mji wa Tunduma jana hayakufunguliwa.


## Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya epaper.ippmedia.com utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza "subscribe"
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa kadi ya benki malipo kwa mtandao wa simu unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa namba ya simu unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. Kwa benki unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

6. Unafungua website yako ya www.ippmedia.com upande wa kulia utaona "E-Paper" utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

# TAKUKURU: Kugawa fedha, nguo katika uchaguzi ni kudhalilisha utu

**Na Restuta James**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) imekutana na wanaharakati kujadili namna ya kudhibiti vitendo vya rushwa katika uchaguzi ujazo ili kuhakikisha unakuwa huru, haki na usiogubikwa na vitendo vya rushwa.

Vilevile, imeonya kugawa fedha, nguo na chakula kwa wapigakura ili wasipige au wamchague mgombea fulani, ikisisitiza kuwa hali hiyo inadhalilisha utu na kunyima wananchi haki ya kupata viongozi waadilifu.

Akifungua warsha ya wadau kutoka Asasi za Kiraia (AZAKI) na Asasi Zisizo za Serikali (AZISE), jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU, Kamishna wa Polisi Salum Hamduni, alisema taasisi hiyo itashirikiana na wadau ili Uchaguzi wa Serikali za Mitaa uliopangwa kufanyika mwaka huu na Uchaguzi Mkuu mwakani uwe wa kidemokrasia.

Alisema TAKUKURU, AZAKI na AZISE wamekutana kujadili na kuweka mkakati wa pamoja ili kuzuia na kupambana na rushwa wakati wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka huu na Uchaguzi Mkuu mwakani.

"Vitendo vya rushwa katika uchaguzi vinasababisha kuwa na uchaguzi usiozingatia misingi ya haki na usawa; na hili imekuwa tatizo la kidunia. Hata Tanzania haijaachwa salama. Tatizo hili limeifanya TAKUKURU kuendelea kubuni mikakati ya kuikabili rushwa katika uchaguzi kwa kuwa madhara yake ni makubwa sana," alisema.

Kamishna Hamduni alisema: "Rushwa katika uchaguzi ina madhara mengi sana, madhara hayo ni pamoja na upatikanaji viongozi wasio waadilifu, wanaojihusisha na vitendo vya rushwa pamoja na kutozingatia misingi ya haki, usawa, uwazi, uwajibikaji na uzalendo mambo ambayo ni muhimu katika ustawi wa wananchi.

"Rushwa inadhoofisha utawala bora na demokrasia, ambapo baadhi ya wananchi wenye sifa za uongozi bora hushindwa kugombea au kutoteuliwa na kutochaguliwa kwa kuwa hawajatoa hongo," alifafanua.

Kamishna Hamduni alitaja athari nyingine za rushwa kwenye uchaguzi ni uvunjifu wa amani kutokana na migogoro ya kisiasa, nchi kugubikwa na rushwa, wananchi kukosa imani na serikali na hata kusababisha machafuko.

"La kusikitisha zaidi ni kudhalilisha utu kwa kufananisha thamani ya mtu na hongo (fedha, nguo, chakula), anayopewa ili apige au asipige kura.

"Kutokana na ukubwa wa athari zinazoweza kusababishwa na vitendo ya rushwa katika uchaguzi, TAKUKURU imeona ni busara kukutana nanyi kwa lengo la kujadili tatizo la rushwa katika uchaguzi, madhara yake na kisha kuweka mikakati ya pamoja ya kuzuia na kupambana nayo kabla madhara hayajatokea," alisema.

Alisema asasi za kiraia zimekuwa mstari wa mbele katika kutetea haki na usawa, kuelimisha na kuhamasisha wananchi kutambua haki na wajibu wao katika masuala ya kijamii, kiuchumi na kisiasa ikiwamo kushiriki katika uchaguzi pamoja na shughuli za maendeleo, hivyo wanayo nafasi ya kusaidia vita dhidi ya rushwa.

"Ukaribu huu mlionao kwa jamii unawafanya kuwa kundi muhimu sana ambalo linaweza kusaidia kuandaa mkakati wa kudhibiti vitendo vya rushwa kwenye uchaguzi.

"TAKUKURU inaamini ushiriki wenu katika kuandaa mkakati wa kudhibiti vitendo ya rushwa kwenye uchaguzi una faida kubwa, ikiwamo kuchaguliwa kwa viongozi bora watakaoongoza kwa mujibu wa sheria na kutekeleza mipango ya maendeleo," alisema.

Aliongeza kuwa TAKUKURU kupitia Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Sura 329, imejizatiti kuzuia na kupambana na rushwa katika uchaguzi kwa kuelimisha umma kuhusu madhara ya rushwa ili uchague viongozi waadilifu.

Kamishna Hamduni alisema, "Ninaamini kupitia warsha hii tutaweza kuja na makakati kabambe wa kudhibiti rushwa katika uchaguzi... ni rai yangu kwenu kuwa mtumie warsha hii kama fursa muhimu sana ya kuijenga Tanzania ambayo viongozi wake wamepatikana bila kujihusisha na vitendo vya rushwa."

Mkurugenzi Mtendaji wa Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), Lilian Liundi, alisema vitendo vya rushwa vimekosesha wananchi fursa ya kupata viongozi bora na kwamba mkakati wa TAKUKURU utawasaidia wanawake kupata nafasi ya kuteuliwa kuwania nafasi za kisiasa katika ngazi mbalimbali mwaka huu na mwakani.

Mwenyekiti wa AZISE, Lilian Badi, alisema wanaharakati watashirikiana na TAKUKURU kuelimisha umma kuhusu athari ya vitendo vya rushwa kwa lengo la kupata viongozi bora.


## KUMBUKIZI YA MAMA YETU RUTH KARASHANI BULUDA



RUTH KARASHANI BULUDA
(27.6.2022 – 27.6.2024) MIAKA 2

Imetimia miaka miwili sasa, toka ulipoachana nasi na kutwaliwa na Muumba. Kimekuwa ni kipindi kigumu sana katika maisha yetu, ila sala, upendo na ushirikiano kati yetu kwa ujumla wake vimeendelea kutuimarisha na kutufanya wamoja.

Ni mengi mema na mazuri ulitufundisha, kutuasa na kutushauri. Haupo nasi kimwili, ila tunajitahidi kadri tuwezavyo kuenenda katika njia sahihi uliyotufunza na kutuelekeza.

Funzo kuu ambalo tunajivunia umetuachia kama familia ni kuishi kwa kupendana, kuvumiliana katika mapungufu yetu na kuwa na uthubutu katika kupanga na kutekeleza malengo sahihi ya kimaendeleo katika Maisha yetu.

Unakumbukwa na Mumeo Augustino Buluda, Wanao, Wajukuu, Wakwe, Ndugu, Majirani na Marafiki.

Bwana ametoa Bwana ametwaa, Jina lake lihimidiwe.

**Amina**



NSSF
Tunajenga Maisha Yako ya Sasa na Baadaye

## TAARIFA KWA UMMA

**MSAMAHA KWA WAAJIRI WENYE MALIMBIKIZO YA MICHANGO NA TOZO ITOKANAYO NA UCHELEWESHAJI WA MICHANGO**

**Dar es Salaam, tarehe 19 Juni 2024**

MFUKO WA TAIFA WA HIFADHI YA JAMII (NSSF) UNAPENDA KUUTANGAZIA UMMA NA WAAJIRI WOTE KWAMBA UNATOA MSAMAHA WA JUMLA KWA WAAJIRI WENYE MALIMBIKIZO YA MICHANGO NA TOZO KWA KUZINGATIA MASHARTI YAFUATAYO;

1) Waajiri watakaolipa malimbikizo yote ya michango ya wanachama wanayodaiwa na Mfuko kabla au ifikapo tarehe **31 Julai, 2024** na kuendelea kulipa michango kwa wakati ifikapo tarehe **31 Julai, 2024**; watasamehewa tozo zote wanazodaiwa kwa asilimia 100.

2) Waajiri watakaolipa malimbikizo yote ya michango ya wanachama wanayodaiwa na Mfuko kabla au ifikapo tarehe **31 Agosti, 2024** na kuendelea kulipa michango ya wanachama kwa wakati watasamehewa tozo zote wanazodaiwa kwa asilimia 75.

3) Waajiri wote ambao hawana malimbikizo yoyote ya michango wanayodaiwa na Mfuko mpaka kufikia tarehe **31 Mei, 2024** na kuendelea hadi tarehe **31 Julai, 2024** watasamehewa tozo zote wanazodaiwa kwa asilimia 100.

Kipindi kitakachohusika na msamaha huu uliotolewa kwa waajiri kulipa madeni yao yote wanayodaiwa kitadumu kuanzia tarehe **01 Juni, 2024** mpaka tarehe **31 Agosti, 2024.**

Kwa maelezo zaidi wasiliana nasi kupitia simu ya bure **0800116773** au tembelea ofisi ya NSSF iliyo karibu nawe.

**Imetolewa na:**
**Kitengo cha Uhusiano na Elimu kwa Umma**

HABARI KITAIFA

# Serikali yapeleka dawa za mil. 100/- kliniki ya Makonda

**Na Beatrice Shayo,** ARUSHA

SERIKALI imetoa dawa zenye thamani ya zaidi Sh. milioni 100 kwa ajili ya wananchi wanaojitokeza kupatiwa matibabu katika kambi ya madaktari bingwa na wabobezi mkoani Arusha.

Kukiwa na hatua hiyo serikalini, foleni imezidi kuwa ndefu kwa wananchi waliojitokeza katika kambi hiyo, serikali ikiongeza madaktari 20 waliotoka Marekani. Pia kuna mpango wa kuongeza madaktari 100 kati ya leo na kesho.

Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda alibainisha hayo jana alipozungumza na wananchi waliojitokeza kufanyiwa matibabu kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, jijini.

"Kipekee ninaomba tumshukuru Rais Samia Suluhu Hassan, hivi tunavyoongea kuna gari linakuja, lina dawa zenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 100.

"Dawa hizo ambazo Rais Samia amezitoa kupitia Bohari ya Dawa (MSD), ziko njiani, mpaka saa tisa watakuwa wamefika hapa," alisema.

Makonda alisema wamepatiwa vijana wa kujitolea wanaotoka Marekani wanaosomea udaktari na uuguzi, wapo zaidi ya 20, hivyo wanaendelea kuongeza nguvu ili kuhakikisha foleni inakuwa fupi.

Mkuu wa Mkoa, Makonda aliomba radhi wananchi hao kwa usumbufu wowote walioupata katika kupata huduma ya matibabu hayo.

"Ninaelewa ya kwamba kila aliyefika hapa hakutarajia kupata usumbufu, alitegemea angefika na kutibiwa na kisha kuondoka, lakini kutokana na wingi wa watu na mwitikio mzuri, changamoto lazima iwe sehemu ya maisha yetu.

"Ombi langu kwenu tuendelee kuwa wavumilivu, safari ya matibabu si safari nyepesi. Jambo la kwanza tuendelee kuwa wavumilivu ili tufike lengo letu la matibabu," alisema.

Makonda alisema kuwa matibabu yoyote ni eneo ambao linahitajika usikivu, umakini na utulivu kwa kuwa linahitaji utaalamu wa hali ya juu.

Alisema wakifanya haraka katika tiba, kuna hatari mtu akapewa dawa ambazo si za ugonjwa husika au kupimwa kipimo ambacho hakihusiani na tatizo ulilokuwa nalo.

"Kuna wakati unataka upimwe haraka uondoke, tunaomba wananchi mvumilie msikilize daktari, fuata maelekezo yake.

"Kwa mfano, kwenye kitengo cha moyo ile mashine inatumika kupima na kuna muda inahitajika kupumzika, inapopumzika usilaumu, kwenye afya tusiwe na haraka," alisema.

Makonda alibainisha kuwa Jumatatu walitibu wagonjwa 2,034 na juzi walihudumia 4,400, hivyo kwa siku hizo mbili, wamehudumia watu 6,434.

Alisema tayari wameanza mchakato wa kutafuta mabanda na madaktari wengine ili kuongeza kasi ya kutoa huduma kwa wananchi.

Alisema kuna wagonjwa ambao wanabainika wanatakiwa kupelekwa kwenye kipimo cha MRI, kinagharimu zaidi ya Sh. 500,000, serikali inabeba gharama hizo kwa kila mgonjwa anayefanyiwa huduma hiyo.

"Kwa mkoa wetu wa Arusha kipimo hicho kipo hospitali binafsi ya NSK. Kuna watu tumewapaleka wanaendelea kupimwa na wagonjwa 30 wamepewa rufani kwenda Taasisi ya (Moyo) Jakaya Kikwete (JKCI), jijini Dar es Salaam, matibabu yao yatagharamiwa na Rais Samia," alisema Makonda.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi Mifupa na Mishipa ya Fahamu Muhimbili (MOI), Dk. Lemeri Mchome, alisema mwitikio ni mkubwa, wameshaona wagonjwa zaidi ya 600 kwa siku mbili na kwa jana walijiandikisha wagonjwa 500.

Alisema kuna jambo jipya ambalo wamejifunza la kushirikiana na Kanda ya Kaskazini kuhakikisha huduma za kibingwa na kibobezi zinawafikia wananchi wa mikoa hiyo.

"Kwa wale ambao wanahitaji matibabu zaidi tunawapeleka katika hospitali zetu na wale ambao wanahitaji matibabu ya kibingwa tumechukua taarifa zao ili tuwasaidie.

"Kama wanaweza kuja Dar es Salaam, tutawapatia matibabu, kama hawataweza sisi tutapanga kuwafuata Arusha," alisema

Baadhi ya wananchi waliojitokeza wamelalamikia foleni kubwa katika kupatiwa matibabu na wengine wakiishia kuchukua namba na kuondoka nyumbani ili warejee uwanjani huko siku nyingine.

Mwanaisha Hamis (68), alisema amepatiwa namba ya 4,800 na amekuwa kwenye foleni tangu alipofika jana saa 10 alfajiri na hakuwa na uhakika wa kumwona daktari kutokana wingi wa watu.

Swahiba Msechu, mkazi wa Arusha, alisema alifika jana saa 11 alfajiri na mume wake Eresto Mkwizu. Hadi saa nane alasiri walikuwa hawajafanikiwa kumwona dakatri huku wakikumbana na changamoto ya jua kali wakati katika mstari wa foleni ya kumwona daktari.





KWA USALAMA WA TANZANIA IJAYO

Miaka 5 ya Benkibima (Bancassurance), Ujenzi wa Sekta Inayoshamiri na Kupanua Upatikanaji wa Huduma za Bima Nchini

Sekta ya bima nchini inakua kwa kasi kubwa. Katika kuelezea mafanikio hayo Kampuni ya The Guardian Limited (TGL), itachapisha matoleo maalum katika magazeti yake ya **The Guardian** na **Nipashe** mwezi ujao yatakayojikita kuangalia upatikanaji huduma za bima zenye matokeo chanya kwa jamii na taifa kwa ujumla.

Matoleo hayo yatajikita zaidi kuelezea:

- **Mafanikio ya Benkibima kwa Kipindi cha Miaka Mitano**
- **Jitihada za Kitaifa Kupanua Upatikanaji wa Huduma za Bima**
- **Mwelekeo wa Sekta ya Bima katika Serikali ya Awamu ya Sita**

Mradi huu wa ujumuishi wa huduma za kifedha ni jukwaa linalotoa fursa ya kipekee kwa watoa huduma za bima na wadau wengine kuonesha jinsi wanavyochangia ongezeko la upatikanaji huduma za bima na mapokeo yake nchini.

Usikose kutumia nafasi hii adimu kunadi taasisi yako na suluhisho bunifu dhidi ya majanga.

**Ili kupata maelezo zaidi ya jinsi ya kushiriki:**
**Wasiliana nasi kwa simu: 0714 791747, 0763214317, 0753 01427**
**Barua Pepe: advertise@guardian.co.tz**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Jamii jiepusheni matumizi ya dawa bila ushauri

**HIVI** karibuni wataalamu wa afya wameihadharisha jamii, kuhusu matumizi holela ya dawa za maumivu, ambayo mara nyingi watu huamua kujinunulia katika maduka ya dawa.

Dawa hizo ni maalumu kwa ajili ya kutuliza maumivu ya muda au sugu, kama vile wanaougua selimundu na waliotoka kufanyiwa upasuaji.

Mtaalamu kutoka Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe (MNMHH), amebainisha dawa kadhaa ambazo baadhi ya vijana hususan wanafunzi wa shule za msingi na sekondari, huzitumia bila ushauri wa kitabibu.

Vijana hao, hufika katika maduka yanayotoa huduma za dawa za binadamu, wakinunua lengo lao ni kustarehe. Matumizi hayo hugeuka kuwa uraibu na kuwaingiza vijana katika kundi la matumizi ya dawa za kulevya.

Dawa za kulevya ni kemikali ambazo huingia katika ubongo na kumwathiri mtumiaji, kusababisha fikra, hisia, kuleta matendo tofauti kwa matarajio ya umma.

Wapo ambao huzitumia dawa za kulevya kwa njia ya kula/kunywa, kuvuta au kujidunga. Hatua ambayo ni hatari kiafya, hasa kwa kundi la vijana ambalo analitaja ni kuanzia umri wa shule hadi miaka 40.

Tabia ya kununua dawa za kutuliza maumivu kiholela na matumizi ya dawa hizo kwa zaidi ya siku 14 huwa ni uraibu na inaweza kumfanya mtumiaji kutaka kuitumia kila siku.

Uchunguzi wa hospitali hiyo umebainika zaidi ya vijana 600 wanawahudumiwa ili kuwaponya na athari za uraibu ikiwamo matumizi ya dawa hizo hata dawa za kulevya kama bangi. Asilimia 80 hadi 90 ya wenye uraibu wanaotibiwa hospitalini hapo umri wao ni kati ya miaka 16 hadi 40.

Wanapohojiwa ama kufanyiwa tathmini kabla ya kuanza tiba wanabainika kwa asilimia 50 wameanza kutumia dawa za kulevya wakiwa shule ya msingi, sekondari na wachache wakiwa kazini.

Miongoni mwa dawa za kulevya ambazo wanabainika huzitumia ni pamoja na hizo za kutuliza maumivu, ambazo mtaalamu anafafanua kwamba utumiaji holela wa dawa za kutibu maumivu ni kinyume cha malengo na kugeuka kuwa uraibu.

Mirungi, cocaine nazo imebainika vijana hao hutumia.

"Hospitalini kuna dawa ambazo mtu anaandikiwa kutokana na changamoto ya maumivu kwa muda mrefu. Matumizi ya muda mrefu kama wiki mbili wa dawa kama valium, tramadol ni uraibu.

Zipo dawa ambazo zimeruhusiwa kutumika kwa utaratibu, kinyume chake kinaweza kuleta uraibu.

Kiwango hicho cha vijana ambao wanapatiwa tiba hospitalini hapo wapatao 600 ni idadi kubwa ambayo, inategemewa na taifa katika uzalishaji hasa ambao wana umri wa zaidi ya miaka 18.


Kadhalika vijana walio na umri wa kuwa suleni hadi ngazi ya vyuo, walijiingiza katika uraibu huo, hulisababishia taifa hasara kwa sababu muda wao mwingi huutumia kutumia dawa za kulevya badala ya kukuza uchumi.

Kukua kwa teknolojia, tangu miaka ya 2000 hadi sasa kunatajwa sababu kwa baadhi vijana kutumia ukuaji huo tofauti na malengo, kama vile kuwa chanzo cha ubunifu, fursa na ajira kwa kundi la vijana ambalo nchini ni zaidi ya asilimia 60.

Ni vyema vijana ambao baadhi huiga tamaduni zilizo kinyume na maadili, imani kupitia teknolojia tofauti, wabadili dhana hizo kwa kuacha kujikita katika starehe za muda mfupi ambazo ni hatari kwao na taifa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita. 0713 578284,
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Trafiki wafanye kazi zao, wajali pia haki za abiria

**KABLA** sijaanza kuandika nilichokusudia nianze kwa kuwapongeza Askari wa Usalama Barabarani, kwa kazi nzuri wanayoifanya kulinda usalama wa magari na watembea kwa miguu.

Muda wa asubuhi pamoja na jioni kumekuwa na magari mengi nchini, hasa maeneo ya mijini, askari hao maarufu kama trafki wamekuwa wakijitahidi kupunguza msongamano na magari.

Ni muda ambao trafiki hawatumii teknolojia ya taa, bali wanatumia sasa ubinadamu kwa kuruhusu magari yanayopita barabara kuu dakika nyingi zaidi kuliko zile zinazochepuka.

Hiyo inasababisha kupitisha magari mengi ambayo yanakuwa barabara kuu, hivyo kwa kiasi kikubwa kupunguza foleni, tofauti kama wangeacha taa zitumike ambazo zenyewe zimesetiwa kwa uwiano sawa, hazijui barabara kuu, wala ndogo.

Matrafiki, pia wamekuwa wakisaidia sana maeneo ambayo taa zimeharibika. Umeshawahi kuona balaa la sehemu ambazo taa zimeharibika na kuna barabara mbili zinakutana?

Kila dereva hujifanya anajua na mbabe sana kuliko mwenzake. Kila mmoja anataka kuwa wa kwanza kupita na kila mmoja hakubali kumpisha mwenzake.

Matokeo yake magari yanazuiana njia, inafikia hatua hakuna lolote ambalo linaweza kupita, kwa sababu zinakuwa zimefungamana.

Kwa sababu magari ya pande zote yanashindwa kupita na kusababisha foleni ndefu isiyokuwa na sababu yoyote, ambayo haina uhakika kuwa magari yataondoka hapo saa ngapi kwa sababu hakuna tena sehemu ya kupita.

Yaani, hapo sasa mpaka tena atokee, trafiki na kwa ufundi na utaalam wao wanajua waanze kuondoa gari lipi ili mengine yapate njia ya kujinasua, hatimaye barabara zifungke na yaanze kupita. Siwezi kukamilisha pongezi zangu, bila ya kuwapongeza baadhi yao kuwa marafiki wa madereva badala ya kuwa kama maadui.

Tulikuwa tunashuhudia zamani askari wa usalama barabarani walivyokuwa wakiyakamata magari, huku wenyewe wakiwa wamekunja sura na kuwa wakali kwa madereva, lakini kwa sasa wengine wao wameshaondoka huko.

Tunashuhudia trafki analisimamisha gari, mfano daladala, anatoka dereva au konda anakwenda kwake, wanaongea kwa namna ya kirafiki, wanacheka, anaonyeshwa makosa yake, wanamalizana, anarudi akiwa anatabasamu.

Hata hivyo, kuna kitu kimoja ambacho kinawakwaza abiria kwenye daladala. Baadhi ya trafiki, wanakamata daladala na kuziweka muda mrefu bila kuziruhusu. Ikumbukwe kuwa abiria wanakuwa kwenye mizunguko ya maisha yao ya kila siku, baadhi wakitakiwa kuwahi.

Kuchelewa kwao kunaweza kusababisha matatizo makubwa kwao na hata huko wanakokwenda.

Wapo wanaowahi kazini, ambapo kuna ofisi zingine ukipitisha hata dakika moja tu baada ya muda uliowekwa hauruhusiwi tena kuingia, unakatwa mshahara au kupigwa memo.

Kuna wanaowahi hospitalini, ambako wanapelekea wagonjwa chakula na muda uliopangwa hawaruhusu tena kuwaona au kupokea msosi.

Wapo wanaowahi muda wa ahadi waliopeana na wapenzi wao, wanaochelewa inakuwa kwao, wanawakosa au kuwakuta wamefura kwa hasira. Usione watu wamo ndani ya daladala, ukadhani hawana haraka.

Nimeshuhudia daladala limesimama kituoni kupakia abiria likichukua dakika kadhaa, lakini wakati linaondoka tu, likasimamishwa na trafki ambaye alikuwa hapo hapo analitazama bila kulikamata, badala yake akasubiri liondoke kwanza, na kusababisha mshangao kwa abiria wote ambao walilazimika kukaa tena dakika zingine pale pale.

Mimi nadhani siku hizi hakuna ulazima wa madereva kusimamishwa muda mrefu kwa sababu wana mashine za faini za kieletroniki.

Wakati wakifanya kazi, waangalie pia haki za wengine hasa magari yenye abiria ambayo yanakuwa na watu wengi wenye haraka, wakiwemo wagonjwa pia wanaowahi hospitali.

# UN Women yalia na idadi ndogo mabalozi wanawake

**Na Christina Mwakangale**

SHIRIKA la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia masuala ya Wanawake (UN Women) limesema kuna idadi ndogo ya mabalozi na wawakilishi wanawake duniani.

Kwa mujibu wa shirika hilo, wastani uliopo kwa sasa kwa kundi hilo, ikiwa wastani wa asilimia 21 katika nchi 193.

Shirika hilo limebainisha kuwa katika nchi 193 wanachama wa Umoja wa Mataifa (UN), marais wanawake ni 34 tu.

Naibu Mwakilishi Mkazi wa UN Women nchini, Katherine Gifford, alisema hayo juzi wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wanawake katika Diplomasia yaliyofanyika jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na mabalozi kadhaa wanaoziwakilisha nchi zao nchini.

Alisema wakati Tanzania angalau imefikia usawa kwenye uongozi, bado uwiano wa uongozi ni mdogo duniani na itachukua takribani miaka 40 kufikia hatua hiyo.

"Wakati maendeleo yamepatikana Tanzania na mengine mengi, uwiano wa kimataifa wa wanawake katika ofisi za kisiasa uko chini katika usawa, kwa kasi ya sasa ya maendeleo inakadiriwa bado uwakilishi bungeni hautapatikana hadi mwaka 2062.

"Katika diplomasia hadi mwaka 2023, wanawake ni asilimia 21 tu ya mabalozi na wawakilishi wa kudumu duniani kote. Hii inadhihirisha kwamba bado tuko mbali na usawa katika nyadhifa za juu za kidiplomasia.

"Kati ya nchi 193 wanachama wa UN, ni wanawake 34 pekee wanaohudumu kama wakuu wa nchi au serikali waliochaguliwa," alisema Katherine.

Alisema matumaini ni kwamba mkutano huo utajikita kujadili changamoto za kipekee wanawake wanakabiliana nazo na kujenga mazingira jumuishi ili kusaidia kupanda kwenye nafasi za uongozi.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Zanzibar, Riziki Pembe Juma, alisema mafanikio yamo nchini, ikiwamo elimu kwa wote bila kumwacha nyuma msichana.

"Tumeimarisha huduma ya afya mama na mtoto, kuwezesha wanawake kiuchumi. Tanzania ndio ushahidi wa kwanza kwamba tunasimamia usawa wa kijinsia na kufikia malengo ya kidunia katika kuweka wanawake katika uongozi kuhakikisha sauti zao zinawakilishwa," alisema.

Aliongeza kuwa Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan pia inahimiza matumizi ya nishati safi ya kupikia, ikiwekeza Sh. bilioni 2.2 ili kuinua jamii husasan wanawake ambao ndio wahusika wakuu wa masuala ya upishi.



Mwenyekiti wa Umoja wa Viongozi wa Afrika katika Mapambano dhidi ya Malaria (ALMA), Sissoco Embaló ambaye ni Rais wa Guinea Bissau (kulia), akijipiga picha alipotembelea ofisi za ALMA, jijini Dar es Salaam hivi karibuni. Wa pili kulia ni Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Jaji: Daktari huyu afunguliwe kesi ya jinai

**Na Grace Gurisha**

JAJI wa Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam, Hamidu Mwanga, ameshauri Dk. Martha Tsere, ambaye anadaiwa kughushi fomu ya bima ya maisha ya rafiki yake wa karibu, afunguliwe kesi ya jinai.

Dk. Matha anadaiwa kughushi fomu ya bima ya maisha ya rafiki yake, marehemu Tarsila Oisso, akidai kuwa anatakiwa apewe asilimia 40 ya bima hiyo.

Katika shauri hilo la madai namba 11290 la mwaka 2024, mlalamikaji ni Shirika la Usimamizi wa Maendeleo kwa Afya (MDH) na Kampuni ya udalali wa bima ya Busara.

Walifungua shauri hilo dhidi ya Dk. Martha ambaye ni mfanyakazi wa MDH pamoja na msimamizi wa mirathi ya Tarsila, Justine Edwald (kaka wa marehemu).

Jaji Mwanga alitoa ushauri huo juzi kwa shirika hilo na kampuni hiyo ya bima baada ya kupitia maelezo ya awali ya kesi hiyo pamoja na kusikiliza hoja (mabishano) ya pande zote kama shauri hilo ni la kuingiliana (interpleader suit).

"Ninaashauri, kesi hii ina tuhuma kubwa za kughushi, kwa maana hiyo ni vyema kufungua kesi ya jinai ya kughushi," alisema Jaji Mwanga.

Katika shauri hilo, Dk. Martha kupitia mawakili wake, Water Chipeta na Saimon Lyimo, amejibu maombi yaliyowasilishwa na wadai hao kwamba anastahili kulipwa asilimia 40 ya bima ya maisha ya marehemu Tarasila.

Pia anadai kwamba kesi iliyoko mahakamani imekosewa, hivyo ameweka mapingamizi mawili ya awali ambayo yatasikilizwa Agosti 22, 2024 mbele ya Jaji Mwanga.

Katika mapingamizi hayo, Dk. Martha anadai kuwa kesi hiyo haikupaswa kuletwa kwa 'interpleader suit', anaomba itupiliwe mbali na pia ni matumizi mabaya ya mahakama.

Shirika hilo limefungua madai dhidi ya Tsere na Edwald ili mahakama iamue nani anastahili kulipwa bima hiyo ya maisha na kwa kiwango gani.

Katika fomu ya warithi ya Group Life Insurance, inadaiwa Dk. Martha anataka alipwe asilimia 40 ya kiwango cha fedha cha bima hiyo ambacho ni Sh. 478,557,322.00.

Upande wa dalali wa bima hiyo na MDH, unadai kupata wasiwasi "inakuaje mtu asiye ndugu kupewa kiwango hicho cha fedha bila ushahidi wowote?" Hivyo, ukahitaji uthibitisho zaidi kama kweli marehemu aliandaa fomu hiyo au la.

Katika fomu hiyo ya madai, inadaiwa kuwa uongozi wa MDH uliamua kushirikisha Jeshi la Polisi Kitengo cha Uchunguzi wa Kisayansi (Forensic Bureau).

Inadaiwa kitengo hicho kilibaini mwandiko na saini katika fomu hiyo si za marehemu Tarsila Oisso, aliyekuwa mfanyakazi wa shirika hilo.

Kutokana na matokeo hayo, Inadaiwa MDH ilipeleka shauri Mahakama Kuu ili chombo hicho kiamue usahihi wa fomu na uhalali wake.

Inadaiwa katika fomu hiyo ya madai kwamba, uchunguzi wa kitengo hicho cha Jeshi la Polisi, ulibaini fomu hiyo ilighushiwa Disemba 16, 2022, jambo linalodaiwa kumsukuma mwajiri kuamua kufungua shauri la kuingiliana (interpleader suit).

MDH pamoja na dalali wa bima hiyo walifungua shauri hilo dhidi ya Dk. Martha na Edwald ili mahakama iamue nani anastahili kulipwa bima hiyo ya maisha na kwa kiwango gani. Mfamasia huyo (Tarsila) alifariki dunia Disemba 21, 2022.

Katika fomu hiyo ya madai iliyoko mahakamani, inadaiwa kuwa fomu ya mgawanyo wa bima ya maisha ya Tarsila ilighushiwa wakati ambao mfamasia huyo alikuwa katika Chumba cha Uangalizi Maalum (ICU) cha moja ya hospitali kubwa jijini Dar es Salaam ambako alikuwa anapata matibabu ya maradhi yaliyokuwa yanamsumbua.

## KABWELA

**Na Fadhil Mohammed**



HABARI KITAIFA

# Dola milioni 112 kutekeleza shughuli za maendeleo EAC

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

BUNGE la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EALA) limewasilisha makadirio ya bajeti yake kwa mwaka 2024/25 ya Dola za Marekani milioni 112, kwa ajili ya shughuli za maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na taasisi zake.

Akiwasilisha makadirio ya bajeti hiyo jana jijini hapa katika mkutano wa nne wa Bunge hilo, Mwenyekiti wa Baraza la Mawaziri, Deng Kuol, alisema bajeti hiyo itasaidia kuendesha shughuli mbalimbali za maendeleo za jumuiya hiyo na taasisi zake.

Alisema bajeti hiyo itasaidia kupeleka ajenda ya ufanyaji biashara pamoja na mchakato wa kutia saini itifaki mbalimbali za EAC.

Baada ya kuwasilishwa kwa makadirio hayo, Mbunge wa Tanzania, James Ole Millya, alisema Tanzania ina mahitaji mengi na shida hazijawahi kuisha, lakini iko mstari wa mbele kuchangia michango yake kwa jumuiya.

"Inatulazimu sisi Tanzania, kuomba fedha kwa wadau wa maendeleo, lakini hatujawahi kuacha kuchangia michango yetu kwa jumuiya hii kwa asilimia 100 kadhalika kwa nchi za Uganda na Kenya.

"Ninapata shaka kwa nchi zingine, zinasuasua uchangiaji wake na kusababisha hali ngumu ya utekelezaji bajeti ya jumuiya," alisema.

Mbunge Fatma Ndagiza kutoka Rwanda alisema kuwa wajumbe wa Kamati ya Bajeti ya Bunge hilo, yeye ni mmoja wao, waliketi kwa wiki mbili kuichambua na kuweka vipaumbele vyao kuhakikisha inatumika vizuri pamoja na kwamba bajeti haitoshelezi.

Abdullah Makame kutoka Tanzania alisema pamoja na usomwaji wa makadirio ya bajeti hiyo, kuna tatizo la kusuasua kwa baadhi ya nchi wanachama kutoa michango yake katika jumuiya hiyo kama inavyotakiwa.






Msimamizi wa Ada na Tozo wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Canisius Karamaga, akizungumza na waandishi wa habari, Dar es Salaam jana, kuhusu tozo na ada mbalimbali ambazo wawekezaji wanapaswa kulipa. Kushoto ni Meneja Mawasiliano wa NEMC, Irene John. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# NEMC yaonya wacheleweshaji malipo ya tozo za mazingira

**Na Joseph Mwendapole**

BARAZA la Taifa la Uhifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limeelekeza wawekezaji wa miradi mbalimbali kulipa tozo na ada za mazingira wanazodaiwa kabla ya kupigwa faini kwa kushindwa kuzilipa kwa wakati.

Msimamizi wa Tozo na Ada mbalimbali wa baraza hilo, Canisius Karamaga, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam.

Alisema ada hizo ni muhimu kwa ajili ya kuliwezesha baraza kutekeleza shughuli zake za msingi lilizopewa kisheria na kuwawezesha wananchi kuwa salama kwa kufanya tathmini ya athari kwa mazingira kabla ya miradi kuanza.

"Tozo hizi ndizo zinasaidia NEMC kutekeleza majukumu yake kwa wakati. Kwa mfano, tunapopata taarifa ya mafuriko au kimbunga, maofisa wetu wanakwenda kuangalia maeneo husika na kufanya tathmini ya kina," alisema.

Karamaga alisema kuwa baada ya tathmini hiyo, huishauri serikali hatua za kuchukua kuepusha maafa na kazi hizo zote zinafanywa kutokana na ada na tozo hizo.

"Lengo la ada na tozo hizo ni baraza lipate fedha ili miradi ikaguliwe, ipate miongozo iliyo sawa na kufanyiwa tathmini ya athari za mazingira na wawekezaji waweze kushauriwa namna ya kuweza kuendesha shughuli zao bila kuathiri mazingira," alisema.

Alisema ada na tozo hizo zina utaratibu na muda wa kulipa kwa mujibu wa sheria na kwamba kinyume cha hapo, wale wanaolimbikiza hukumbana na adhabu ya riba ya asilimia tano kwa kila mwezi kwa mhusika aliyechelewesha malipo hayo.

Alisema tozo husaidia baraza kupata fedha kutoka kwa wanaofanya miradi kuwezesha kukaguliwa na kupata vyeti vya tathmini ya athari kwa mazingira.

"Kwa mfano, mwekezaji akitaka kujenga kiwanda, lazima tumshauri namna gani ya kukijenga na namna ya kufanya tathmini ya athari kwa mazingira, vitu gani afanye na vitu gani asifanye. Sasa yote hayo ni gharama, lazima kuwe na fedha," alisema.

Karamaga alisema nia ya kufanya tathmini ya athari kwa mazingira ni kumwezesha mwekezaji kujenga mradi ambao hautasababisha mgogoro na wananchi wanaoishi jirani na kusababisha madhara.

Pia alisema tozo hulipwa kwa njia mbalimbali na katika kanda 12 za NEMC zilizoko nchini ambapo wahusika wamekuwa wakipewa namba za malipo.

Alisema wananchi wamehamasika kulipa ada na tozo mbalimbali zilizowekwa kwa mujibu wa sheria za nchi. Baadhi wanalipa baada ya kukumbushwa mara kwa mara.

"Wasiolipa kwa wakati tunawaandikia barua, tunawapigia simu, tunawakumbusha kwa njia mbalimbali na wengi huwa wasikivu sana kwa kuwa tukiwakumbusha wanalipa kwa wakati," alisema.

Ofisa huyo pia alisema kuna umuhimu kwa Watanzania kujali na kutunza mazingira kwa kuwa mabadiliko ya tabianchi yamekuwa yanasababisha athari kubwa kwa miundombinu ya nchi na wakati mwingine watu kufariki dunia kutokana na majanga.

"Lazima tuyajali mazingira kwa sababu tukiyapuuza huwa yanatukumbusha umuhimu wake, na ndiyo sababu utaona majanga mbalimbali kama mafuriko, moto, kimbunga na mengine yanayotokana na mabadiliko ya tabianchi," alisema.



# Shule 96 zaanza kutoa elimu ya amali

**Na Allan Isack,** ARUSHA

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Carolyne Nombo, amesema mabadiliko ya sera ya mtaala wa elimu umepokelewa vizuri na wadau wa elimu nchini, kwamba hadi sasa shule 28 za serikali na 68 za watu binafsi zinatoa elimu ya amali.

Prof. Nombo alisema hayo jana jijini Arusha, wakati wa kikao kazi na wadau mbalimbali katika sekta ya elimu hapa nchini, wakiwamo kutoka serikalini na sekta binafsi.

Alisema tangu Januari mwaka huu, wameshaanza utekelezaji wa mitaala ya elimu iliyoboreshwa kwa kuanza na darasa la awali, la kwanza, tatu, kidato cha kwanza mafunzo ya amali, pamoja na wanafunzi watakaojiunga na kidato cha tano mwaka huu watatumia mitaala ya elimu iliyoboreshwa.

"Elimu msingi itahusisha miaka sita ya elimu ya msingi kuanzia darasa la kwanza mpaka la sita na mwanafunzi atasoma mwaka mmoja wa elimu ya awali, lakini mwanafunzi atakapomaliza darasa la sita ataingia kidato cha kwanza na atasoma miaka minne ya elimu sekondari ngazi ya chini.

"Kwa elimu ya sekondari kulingana na muundo mpya mwanafunzi atakuwa na uhuru wa kuchagua kwenda kusoma elimu ya sekondari ngazi ya chini masomo ya jumla au elimu ya sekondari ngazi ya chini masomo ya amali ikimaanisha mafunzo ambayo yatampatia mwanafunzi ujuzi na umahiri wa kufanya kazi," alisema.

Mwenyekiti wa washirika wa maendeleo katika sekta ya elimu, Faith Shayo, alisema lengo la mkutano huo ni kujadiliana masuala mbalimbali ya elimu ili kuhakikisha sekta hiyo inapiga hatua.

Mwenyekiti wa Mtandao wa Elimu Tanzania, Faraja Nyalandu, alisema wakiwa sehemu ya wadau wa elimu wana amini katika ushirikishwaji, mipango na utekelezaji wa hafua zinazokwenda kugusa maendeleo ya sekta ya elimu nchini.

# Bunge la Afrika Mashariki lapata Katibu Mkuu mpya

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA



KATIBU Mkuu mpya wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Veronica Nduva, ameapishwa rasmi kuwa mjumbe wa Bunge la Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (EALA).

Nduva (pichani) aliapishwa juzi baada ya kula kiapo Juni 7 mwaka huu, huko Juba, Sudan Kusini mbele ya wakuu wa nchi wa EAC.

Nduva alitangazwa jana na Bunge la EALA kuchukua nafasi hiyo, ili kuziba pengo la mtangulizi wake, Dk. Peter Mathuki.

Akizungumza katika Bunge hilo jana, Nduva aliahidi kufanya kazi bega kwa bega na bunge hilo kwa ushirikiano ili kufikia malengo Ya EAC.

"Ninatoa shukrani zangu za dhati kwa Jamhuri ya Kenya kwa kuniteua kashika nafasi hii muhimu. Ninajitolea kufanya kazi kwa karibu na ujenzi wa Bunge juu ya msingi thabiti uliowekwa ili kufikia matarajio mazuri yaliyoainishwa katika mkataba,"alisema.

Alisema kwa pamoja wakishirikiana watahakikisha wanaimarisha ushirikiano wa kiuchumi, kisiasa, uwiano wa kijamii na uimarishaji wa kitaasisi.

Aidha, alisema amejitolea kukuza ushirikiano wenye tija na wajumbe wa Bunge na kuimarisha jukumu na mwonekano wa vijana katika jumuiya hiyo, pamoja na kuhakikisha sera zao zinaeleweka vizuri basi ili kuleta maendeleo ya EAC.

Baada ya ukaribisho katika bunge hilo, baadhi ya wabunge wakiongozwa na mbunge wa nchini Uganda, Paul Musamali, wamemWonya kuwa msimamizi mzuri wa rasilimali za jumuiya hiyo.

"Jumuiya haina fedha za kutosha ndio maana tunahitaji usimamie vizuri tafadhali katibu mkuu, usiweke mikono yako huko, kuwa mwaminifu na tutakuunga mkono," alisema Musamali.

Juni 7 mwaka huu, Nduva, alikula kiapo huko Juba nchini Sudan Kusini, mbele ya wakuu wa nchi za jumuiya ya Afrika Mashariki na kuanza rasmi majukumu yake ya Katibu Mkuu kuziba nafasi ya mtangulizi wake Dk. Mathuki.

Vuguvugu la kuondolewa kwake, Dk. Mathuki katika nafasi ya katibu Mkuu wa EAC, lilianzia Machi mwaka huu katika kikao cha tatu cha bunge hilo, huko Nairobi nchini Kenya, ambapo alituhumiwa na baadhi ya wabunge hao kwa ubadhirifu na matumizi mbaya ya madaraka.


# NOTISI / TANGAZO

**LEGENDS AUCTION MART LTD, DESTENI COMPANY LIMITED, NUTMEG AUCTIONEERS & PROPERTY MANAGERS CO.LTD ,SALEI AUCTION MART LTD,HEDANE ENTERPRISES LTD, MASE INTERNATIONAL LTD,TAUSI AUCTION MART,MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTORS, JY AUCTIONEERS CO.LTD,DRM AUCTIONEERS & CO.LTD, MAS AND ASSOCIATES CO.LTD,MELVA INTERNATIONAL LTD ,SUMA JKT AUCTION MART COMPANY LTD,MAJEMBE AUCTION MART LTD, MABUNDA AUCTIONEER MART CO.LTD, TRUST RECOVERIES LTD, BEST GROUP (T) LTD,JAMOK INVESTMENT LTD,MCHINGA AUCTION MART,GADAU AUCTION MART,AMI AUCTION MART, IGALULA AUCTION MART,BAHARI AUCTION MART, ADILI AUCTION MART,KOTI BROTHERS CO. LTD,PROPERTY MASTER LTD,MULTLINK AGENCY LTD,TWINS AUCTIONS MART, BID CITY AUCTION,JALAS AUCTION MART,HOLLYNESS COMPANY LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC,** tunatoa notisi ya kulipa deni kwa mdaiwa, Vinginevyo, tutafanya Minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI ALILOKOPA | JINA LA MTEJA | AINA YA DHAMANA | JINA LA MWENYE DHAMANA | MAHALI DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| DODOMA | DOLUPHA TANZANIA LIMITED | GAR TRALER T105 DSX, SCANIA T203 DXL, SKELETAL TRAILER T258 DWB, SCANIA T162 DSW | DOLUPHA TANZANIA LIMITED | DODOMA | 29/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| KIJITONYAMA | HAFIDH HASSAN HAFIZO | NYUMBA | HAFIDH HASSAN HAFIZO | MWANDEGE- MKURANGA | 9/07/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| KIJITONYAMA | JOSEPH DASTAN BARUA | NYUMBA | JOSEPH DASTAN BARUA | SARANGA | 10/07/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| ILALA | BIAGATI SEA FOODS CO. LTD | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI NAMBA TMK033735 | DAVID ABEL MLAU | CHARAMBE -MBAGALA | 29/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| BUGURUNI | ZAKARIA RETSON SHIMWELA | NYUMBA | ZAKARIA RETSON SHIMWELA | PUGU-KINYAMWEZI | 11/07/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | OMARY ABDALLAH CHINKONDO | NYUMBA | OMARY ABDALLAH CHINKONDO | KIVULE-MAJOHE | 11/07/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | SALVATORY MODESTI NGOWI | NYUMBA | SALVATORY MODESTI NGOWI | KIPUNGUNI 'B'-KITUNDA | 12/07/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| BUGURUNI | ATHUMANI MBWANA KAWESA | NYUMBA | ATHUMANI MBWANA KAWESA | TABATA-MSIMBAZI | 13/07/2024 SAA 04:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| TEMEKE | MNANA AYUBU ABUU | NYUMBA | MNANA AYUBU ABUU | PUGU-KIGOGO FRESH 'A' | 12/07/2024 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MBAGALA | SAID RAMADHANI MWAKITUBU | NYUMBA | SAID RAMADHANI MWAKITUBU | CHATEMBO MWANDEGE | 11/07/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| UKONGA | LAMECK RICHARD RWEYONGEZA | NYUMBA | LAMECK RICHARD RWEYONGEZA | KIVULE-MAJOHE | 28/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UKONGA | MAX AYUBU MBONYE | NYUMBA | MAX AYUBU MBONYE | YONGWE-CHANIKA | 28/06/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| UKONGA | KASA MUSSA SELEMANI | NYUMBA | KASA MUSSA SELEMANI | CHANIKA | 05/07/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA (MARUDIO) |
| MOSHI | VALENTINE MATHIAS SHILIMA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI NA.40137 KIWANJA NA.340 KITALU "A" | VALENTINE MATHIAS SHIRIMA | MOSHI -NJORO | 11/07/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | SCOLASTICA SIRILY TEMBA | NYUMBA | PAUL ELVIS NGOWI | MOSHI -RAU | 12/07/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | JULIUS STANLEY MALYA | NYUMBA | JULIUS STANLEY MALYA | BOMANGOMBE-HAI | 13/07/2024 SAA 4 :00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MOSHI | NEEMA SOLOMONI MWANGA | NYUMBA | NEEMA SOLOMONI MWANGA | BOMANGOMBE-HAI SINAI | 13/07/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | HELENA IGNATUS NYAKARASHI | NYUMBA YENYE HATI MILIKI NA.87634 | GEORGE SLIVESTER ADOGO | NYAMADOKE ILEMELA MWANZA | 11/07/2024 SAA 4:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |
| MWANZA | MASHAKA CHARLES BULUBA | NYUMBA YENYE HATI MILIKI NA.62183 | MASHAKA CHARLES BULUBA | NYASAKA ILEMELA MWANZA | 11/07/2024 SAA 5:00 ASUBUHI NA KUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1 Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya Nyumba, Kiwanja, Gari au Shamba ,papo hapo baada ya mnada kumalizika na 75% itakayobaki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2 Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali,hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3 Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no.0759648448/0784787981/0715363537
4 Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzi hajakabidhiwa nyumba Benki itarudisha kiasi cha fedha kilichowekwa na mnunuzi Benki bila gharama yeyote.



# Taasisi elimu, afya vinara madeni ya maji

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

TAASISI za umma zikiwemo za elimu na afya katika Halmashauri ya Msalala na Ushetu mkoani Shinyanga, zimetajwa kuwa kikwazo katika utoaji wa huduma za maji kutokana na kuwa na malimbikizo makubwa ya madeni wanayodaiwa na Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA).

Kaimu Meneja wa RUWASA Kahama, Paschal Mnyeti, aliyabainisha haya kwenye mkutano mkuu wa mwaka wa wadau wa maji kwa vyombo vya kutolea huduma ya maji ngazi ya jamii, lengo likiwa ni kujadili na kubadilishana uzoefu kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu maji na usafi wa mazingira.

Alisema, taasisi za umma hasa shule za msingi, sekondari, zahanati na vituo vya afya zinaongoza kwa kushindwa kulipa ankra za maji.

Alisema hali hiyo inasababisha kushindwa kutoa huduma ya maji ipasavyo kwenye jami, kwamba fedha zinazopatikana zinatumika kukarabati miundombinu na kulipa gharama za uendeshaji hasa umeme.

Hivyo, aliiomba serikali kuingilia kati na kuzishinikiza ziweze kulipa ankra zinazodaiwa, akisema zipo zinazodaiwa Sh.300,000 mpaka Sh.milioni moja.

Aiisema katika mwaka wa fedha 2023/2024 wameweza kutekeleza miradi mbalimbali ya maji yenye mtandao wa mabomba ya kusambaza maji kwa gharama ya Sh.bilioni 9.4 yenye uwezo wa kuwahudumia wananchi 62,824 katika Halmashauri ya Msalala na Ushetu.

Mkuu wa dawati kwa umma kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Happiness Bilakwate, alisema wamekuwa wakipokea malalamiko ya watumiaji wa maji kubambikiwa ankra za maji.

Alisema hali hiyo inasababisha wananchi kulipa bili tofati na kile wanachotumia, hivyo aliwataka watoa huduma ngazi ya jamii kuacha mara moja tabia hiyo.

Mkuu wa idara ya usanifu wa miradi ya maji na bajeti kutoka RUWASA mkoani Shinyanga, Cyprian Ndabarunye, alisema wamepokea Sh. bilioni 1.5 kwa ajili ya kuchimba visima 27 kati ya 900 vinavyohitajika nchini.

Alisema kwa sasa wanajiandaa kuzifikisha mahakamani taasisi zote za umma pamoja na viongozi ambao ni wadaiwa sugu.

Kaimu Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Julius Mtatiro, alitoa siku 15 mpaka Julai tano kuhakikisha taasisi zote za umma zinazodaiwa ankara za maji kuhakikisha zinalipa madeni.

Aidha, aliagiza RUWASA kumuorodheshea taasisi zote madeni wanayodaiwa bila kuogopa viongozi wenye mabavu, kwani serikali imedhamilia kumtua ndoo mama kichwani.



Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga ambaye anakaimu ukuu wa Wilaya ya Kahama, Julius Mtatiro, akizungumza katika mkutano mkuu wa mwaka wa wadau wa maji kwa vyombo vya kutolea huduma ya maji ngazi ya jamii (CBWSO), ulioandaliwa na Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), wilayani humo mkoani Shinyanga jana, ili kujadili na kubadilishana uzoefu kuhusu masuala mbalimbali yanayohusu maji na usafi wa mazingira. **PICHA: SHABAN NJIA**

## RC akoshwa halmashauri kupata hati safi za CAG

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha, amezipongeza halmashauri tatu za mkoa huo kwa kupata hati safi, kutokana na kujibu hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Alitoa pongezi hizo juzi wakati akizungumza kwenye vikao viwili vya Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga na Manispaa ya Shinyanga.

Alisema kutokana na halmashauri hizo kupata hati safi kutoka kwa CAG ikiwamo na Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, ameona ni vyema akazipongeza ili kuendelea kuwatia moyo watumishi kwa kufanya kazi nzuri na kusimamia vizuri fedha za utekelezaji wa miradi ya maendeleo.



"Wanaofanya vizuri ni vizuri kuwapongeza, ila natoa angalizo hati hizi safi zisije kuwalewesha mkajaa sifa na kusahau majukumu yenu, endeleeni na kasi hiyo ya kuchapa kazi kwa bidii na kumsaidia Rais Samia Suluhu Hassan,"alisema Macha.

Aidha, aliwataka watumishi wa serikali kila mmoja awajibike kwa kutekeleza majukumu yake kulingana na nafasi aliyonayo pamoja na kuendelea kufanya kazi kwa ushirikiano na upendo, ili kuweza kuleta tija na ufanisi na kuchochea maendeleo.

Meya wa Manispaa ya Shinyanga, Elias Masumbuko, aliwasisitiza watumishi waongeze umakini na ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu yao pamoja na kuzishughulikia hoja zinazoibuliwa na CAG ili zipate kufutwa.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga, Nikodemus Simon, alisema madiwani wa halmashauri hiyo wataendelea kushirikiana na wataalamu ili kuchochea maendeleo pamoja na kufuata sheria na kanuni za utumishi na kuendelea kupata hati safi.

## Wamiliki viwanda walalamikiwa kutiririsha maji ya kemikali

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MADIWANI katika Halmashauri ya Msalala mkoani Shinyanga, wamewalalamikia wamiliki wa viwanda vya kuchenjua madini ya dhahabu kutiririsha maji ovyo yenye kemikali ya zebaki, ambayo yanasababisha mifugo kufa pindi wanapokunywa.

Walibainisha hayo kwa nyakati tofauti wakati wakijadili na kutoa taarifa za maendeleo ya kila kata katika kikao cha Baraza la Madiwani cha Halmashauri hiyo.

Diwani wa Kata ya Lunguya, Benedicto Manwali alisema, idadi kubwa ya viwanda hivyo havina uzio na mifumo ya majitaka, hali inayosababisha utiririshaji wa maji hayo kwenye maeneo ya marisho.

Manwali alisema maafa ya mifugo kufa yamekuwa yakijitokeza katika viwanda vilivyopo katika Kata za Lunguya na Segese na kuiomba serikali kuingilia kati na kudhibiti majanga hayo na kuchukua hatua dhidi ya watiririshaji hao.

Diwani wa Viti Maalumu, Hamisa Kalinga alisema hali hiyo inahatarisha pia afya za wananchi hususani katika mfumo wa fahamu, figo, uwezo wa kuona, mikono kutetemeka, mimba kutoka.

Alitaja athari nyingine ni watoto kuzaliwa na utindio wa ubongo na kuchanganyikiwa hivyo kunaulazima wa wamiliki wa viwanda hivyo kudhibitiwa.

Mkuu wa Kitengo cha Maliasili na Uhifadhi wa Mazingira Halmashauri hiyo, Salehe Lyulu alikiri kuwepo kwa hali hiyo na kueleza kuwa tayari ametoa muda wa mmoja kwa wamiliki kuhakikisha wanajenga uzio na mifumo ya maji taka ili kukabiliana na hali hiyo.

ama
ALHAMISI JUNI 27, 2024
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 13

**SAMIA ALIVYODHAMIRIA AFYA TAIFA ... Amwaga mabilioni ya vituo afya 1061 na kambi uzazi hospitalini, magari wagonjwa**



**Kilichoko kwenye thamani ya kliniki katika maisha kila siku**

Ukurasa 14

# Anavyoishi anayepoteza kumbukumbu na elimu kutoka bingwa anayemtibu

**Na Christina Mwakangale**

KUFANYA mazoezi ya kimwili na kiakili kama vile kuangalia televisheni, ni miongoni mwa ratiba zake kila iitwayo leo. Huyu ni Frank.

Hiyo sasa inamsaidia ubongo wake kupata shughuli ya kufanya, kuongeza uwezo wake wa mifumo ya fahamu, ikiwamo kumbukumbu. Kadhalika, uwezo wa kunusa umepungua.

Bingwa Mbobezi wa Afya ya Akili na Mfumo wa Fahamu Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe, Dk. Damas Mlaki, anadokeza, uwezo kumbukumbu hutegemea utimamu wa milango mitano ya fahamu.

Ngozi kuhifadhi kumbukumbu za hisia, mguso. Pua (kunusa), macho (kuona), kinywa (ladha) masikio ili kutunza sauti, kwamba kinachohifadhiwa katika ubongo kwa namna tofauti, kama vile maneno, picha, sauti, matukio na hata hisia.

"Uwezo ukiwa duni wa kuzipata taarifa ambazo zimehifadhiwa ndio changamoto, yaani kama huna uwezo kuziteta, ku-retrieve taarifa, ni tatizo tayari katika ubongo. Ili utengeneze kumbukumbu lazima milango yako ya fahamu iwe sawa.

Frank (si jina lake halisi), mkazi wa Buguruni, jijini Dar es Salaam, anaishi na changamoto kadhaa. Ana tatizo la kumbukumbu kutoweka kwa baadhi ya matukio. Tatizo lilimuanza mwaka 2020.

Muda mfupi baada ya kuhudhuria kliniki, Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Frank, anazungumza na Nipashe, mwishoni mwa wiki.



Mwenye tatizo la kumbukumbu. **PICHA: MTANDAO.**

Ameongozana na mkewe, wamepanga foleni kama ambavyo wagonjwa wengine, wakisubiri kuingia kwa awamu kwa mtaalamu.

Ni mwenye afya kwa mwonekano, umri wa makamo, mwenye umri wa kustaafu. Anabadilishana maneno mawili, matatu na walioketi jirani yake katika benchi. Nao makamo yao, hayatofautiani sana na Frank.

"Umri unavyokwenda ndivyo hiki kinaibuka mara hiki. Inabidi ukubaliane na hali..." Nipashe inajongea karibu. Frank, hakusita kuelezea hali yake, akihamasisha wanakumbwa na tatizo lolote kiafya, wafike hospitalini

"Kuna baadhi ya vitu naona kama vinabadilika katika maisha yangu. Kwa sababu kusema kuugua presha ni muda mrefu. Nimeanza kuugua miaka kama 20 imepita.

"Sasa nahisi baadhi ya ratiba za kila siku kama vile kunywa dawa, kushiriki shughuli zilizopangwa mbeleni, sizikumbuki. Nilifanya uchunguzi na kuanza matibabu Muhimbili nilipobainika kuna kasoro katika ubongo," anasema Frank (68).

Ratiba ya kumeza dawa ikiwamo za presha ni ya kila siku kwa Frank. Kwa sasa ratiba hiyo ipo chini ya usimamizi wa mke wake, ambaye huziandaa kwa kutenga sehemu mapema.

"Kuna wakati naweza nikauliza swali, unakuta watoto na wajukuu wanatazamana, kisha wanacheka! ...'baba au babu fundi si alikuja juzi na akakwambia atamalizia hii kazi...' nimesahau.

Sasa anachofanya mke wangu ni kuniandalia kila siku dawa ambazo nakunywa kwa siku, asubuhi. Kama nameza vidonge sita vya siku, vingine ni nusu huvikata.

Anaweka juu juu ya kabati. Nikiamka mguu wa kwanza pale, kabla sijafanya chochote, nisisahau. Si kila siku ninakuwa nasahau baadhi ya vitu, ila kwa sababu dawa nameza kila siku, mke wangu ameweka angalizo kwa ratiba ni hiyo ili nisisahau kumeza.

Dawa za siku 30 za mwezi huzitenga kila aina ya dawa na siku yake. Yaani, Jumatatu hadi Jumatatu, anaziweka kwa kutenganisha inchi chache juu ya meza. Naye hupita kuhakikisha kama leo Jumatatu, dawa za Jumatatu zimemezwa.

Maana hata akiniuliza jibu linaweza kuwa ndio au hapana. Kama hapana, nikurudia je. Kwa hiyo anaangalia pale alipopanga. Hata akisafiri anaandaa kabisa.

Aidha anaandika kwenye karatasi dogo na dawa labda vidonge aina tofauti nne. Kila siku ina karatasi lake, nikiamka nikiona tu, najua karatasi la juu ndio ya siku ya leo.

Kwa sababu natumia dawa aina tofauti, za kumbukumbu, presha nakunywa pamoja, ratiba inapangwa kila mwezi na mke wangu mara baada ya kutoka kliniki kuchukua dawa."

**WANAOPOTEZA KUMBUKUMBU**

Bingwa Mbobezi wa Afya ya Akili na Mfumo wa Fahamu Hospitali ya Taifa ya Afya ya Akili Mirembe, Dk. Damas Mlaki, anasema wanaopoteza kumbukukumbu wengi wao wana umri wa miaka 60 na kuendelea.

Dk. Damas anayasema hayo wiki iliyopita, kwenye makala maalumu iliyochapishwa na gazeti hili, akiwasilisha mada juzi, kuhusu kiungo hicho, anasema taaluma yake inahusika katika kutibu waliopata maradhi na kuathiri ubongo kama vile kiharusi, ajali.

"Huwa nashughulika na waliopata kiharusi na kupata changamoto ya usikivu na kupoteza kumbukumbu au aliyepata ajali, kisha akapata athari kwenye ubongo na kubadili mwenendo wa kiungo hicho kitabia.

Wagonjwa wengi tunaowaona, wanaopoteza kumbukukumbu wana umri wa miaka 60 na kuendelea. Tumekuwa tukiwaona wagonjwa wenyewe umri chini ya miaka 60 pia.

"Tiba ya tatizo la kupoteza kumbukumbu ipo na kuna sababu nyingi zinazosabisha kupoteza kumbukumbu. Matibabu ya ugonjwa wa kupoteza kumbukukumbu yanategemea chanzo, sababu ya kupoteza kumbukumbu," anasema bingwa huyo.

Anasema, baada ya uchunguzi ili kubaini kisababishi cha kupoteza kumbukumbu , mtaalam anaweza kutoa afua za kibaiolojia zinazohusisha dawa, afua za kuuchangamsha ubongo na afua za kijamii.

"Afua za kijamii zinalenga kushauri mambo mbalimbali yakufanya, ili anayepoteza kumbukumbu aweze kuishi salama katika jamii yake pamoja na kuihusisha familia katika kutoa afua zitakazosaidia hali ya mgonjwa kutengemaa.

Inaendelea Uk. 14

MAZINGIRA

UDZUNGWA NA MAZINGIRA...

# Mkaa wa taka unavyong'arisha maisha kinamama, ukipunguza uvamizi milima

**Na Jenifer Gilla**

WAKATI sehemu kubwa ya jamii ikiamini taka ni kitu cha kuweka mbali na maisha yao kwa kukosa thamani, baadhi wameona ni fursa ya kibiashara, kujiongezea kipato na kuhudumia familia zao.

Mwanamke kutoka Kikundi cha Mazingira katika kijiji cha Mang'ula B, katika Halmashauri ya Mji Ifakara, wilayani Kilombero mkoani, Morogoro, anaeleza wanatengeneza mkaa wa kupikia kwa kutumia taka na kuwauzia wakazi wa eneo hilo.

Matamanio ya wanawake hao yalichochewa na uhaba wa nishati ya kupikia unaokikumba kijiji hicho na vingine vinavyoizunguka Hifadhi ya Milima ya Udzungwa, hata kuwafanya husika kuvamia hifadhi na kukata miti ili kupata kuni.

Mhifadhi Mkuu wa Hifadhi ya Taifa ya Milima ya Udzungwa, Theodora Batiho, anawaeleza waandishi wa habari wanachama wa Chama cha Waandishi wa habari za Mazingira Tanzania (JET), kuwa pamoja na utoaji elimu kwa jamii kuhusu utunzaji rasilimali hiyo, tatizo hilo bado linaendelea, kwa sababu kuu ikiwa ni uhitaji wa nishati ya kupikia.

Anawafafanulia wanachama cha Waandishi wa Habari za Mazingira Tanzania (JET) waliokagua njia ya wanyamapori ya Nyerere Selous-Udzungwa, kushuhudia maendeleo yaliyopatikana katika mchakato wa urejeshaji mazingira.

Anaitaja ni hali inayoathiri mandhari ya hifadhi hiyo, pamoja na bayoanuai yake, kuchochea athari za mabadiliko ya tabianchi, hivyo mikakati ya haraka kudhibiti suala hilo inahitajika, kunusuru eneo hilo kupelekwa nishati mbadala wa kupikia.

Msistizo ulioko ni kuwasaidia wakazi wa vijiji kupata nishati safi ya kupikia kwa bei nafuu, ikiwamo na kuwatafuta wadau wa kushirikiana nao kusambaza nishati hiyo, ikiwamo mitungi ya gesi kwa wakazi wa vijiji vilivyo karibu na hifadhi hiyo.

Katibu wa Kikundi cha Mazingira Group, Restuta Vitalis, anasema alianzisha kikundi hicho mwaka 2021 kikiwa na wanachama wanawake 15, kwa lengo la kuanzisha kiwanda kiwanda cha kutengeneza mkaa huo.

Anasema, ni kikundi kilichokuwa kikitengeneza mkaa kwa kutumia njia ya kizamani ya kutwanga kwa mikono, jambo lililosababisha kutengenezwa mkaa kidogo na wenye viwango vya chini jambo ambalo halikukidhi malego yao.

Restuta anasema, baadaye shirika lisilo la kiserikali la Associazione Mazingira, liliwatafuta na kuwapatia mafunzo ya kutengeneza mkaa huo kitaalam na kuwapa mashine ya kisasa.



Mkaa utokanao na taka ukiandaliwa. **PICHA: MTANDAO.**

Anasema, wanatengeneza mkaa huo kwa kutumia taka ikiwamo majani yaliyodondoka, pumba za mpunga na vumbi la mbao, kisha huzitoa moshi halafu huzichanganya na uchafu wa miwa unaotoka kiwandani ili kugundisha na kutengeneza shepu wanayotaka.

"Tuliamua kuingia katika biashara ya kutengeneza mkaa mbadala baada ya kugundua kuwa miti mingi sana ilikuwa inakatwa na wakazi wa vijiji kwa ajili ya kuni," anasema

Anasema mashine hiyo ina uwezo wa kuzalisha kilo 300 hadi 400 za mkaa kwa saa na kama wakiwa na taka za kutosha wanazalisha tani 3 za mkaa kwa wiki na kuuza kilo moja Sh.500, wateja wakuu wakiwa ni watu wa majumbani na wafanyabiashara wa chakula (mama ntilie).

### HALI YA SOKO

Mwenyekiti Msaidizi wa kikundi hicho, Suna Kassim anajivunia kuwa hali ya soko ipo vizuri kwani kwa siku wana uwezo wa kuuza kilo 500 hadi 600 za mkaa na kukusanya ya mauzo. yasiyopungua Sh .250,000 kwa siku.

Anasema kinachovutia watu wengi kununua mkaa huo kwa wingi ni bei yake kuwa nafuu ya Sh. 500 na matumizi yake kuwa ya muda mrefu ukilinganisha na mkaa wa kuni ambao huanzia Sh. 1000 huku ukiisha kwa haraka.

Faida inayopatikana sasa katika biashara hiyo, hugawanywa kwa wanakikundi na nyingine kuwekwa benki kwa ajili ya maendeleo kama vile kuchukuilia mkopo ya halmashauri ili kuboresha biashara hiyo.

"Mfano mwaka huu tulichukua mkopo wa Sh.milioni 14 katika Halmashauri ya Mji Ifakara ambayo ilituisaidia kununua kifaa cha kuchanganyia malighafi na mashine ya kukaushia mkaa," anasema. Ilivyobadilisha maisha

Mjumbe wa Kikundi hicho, Dibaga Philipo anasema biashara hiyo imeongeza kipato chake na kufanikiwa kusomesha watoto watatu, wawili wakiwa chuo na mmoja akiwa sekondari katika shule binafsi.

Anasema, posho anayopokea katika kikundi hicho anaipeleka kwenye mchezo wa kupeana pesa kwa mwezi na wanawake wenzake na siku akipokea analipia mahitaji na ada ya watoto.

Hapo awali, alikuwa akisomesha watoto wa shida kwa sababu alikuwa akitegemea pesa kutoka kwenye kilimo pekee ambazo hazikutosha, na kulazimika kuingia kwenye mikopo ambayo haikuwa salama kwake kiuchumi na kiafya.

Wakati Restituta anasema kuwa kupitia fedha hizo alimsaidia mume wake katika ujenzi wa nyumba yao kubwa ambayo wanaishia sasa na familia yake.

Anasema kwa sasa wamepeana majukumu na mume wake ambayo yeye anatoa kiasi cha pesa na kulipia ada ya watoto hali iliyoongeza upendo kwa kuwa si mtegemezi wa kila kitu kwa mumewe. Changamoto

Magumu wanayokumbana nayo ni kuwa uwezo wa kiwanda kuzalisha ni mdogo ukilinganisha na mahitaji ya soko na upatikanaji wa taka kuwa mdogo hali inayowalazimu kuingia gharama za kukodi gari kuzifuata mbali.

Mfanyabiashara wa chakula kutoka kijiji cha Mang'ula B, Suzana Fidelis, anasema tangu ameanza kutumia mkaa huo faida katika biashara yake imeongezeka kwa sababu unapatana kwa bei nafuu na anautumia muda mrefu ukilinganisha na wa kuni.

Anasema mkaa wa taka wa Sh.2000 anautumia kwa siku mbili tofauti na mkaa wa kuni ambao alikuwa akinunua wa Sh. 8000 ili aweze kuutumia kwa siku hizo.

"Kwa fungu la Sh. 500 naweza kupikia chapati 60 na bado moto ukaendelea kuwapo, wakati kwa mkaa wa kuni ningetumia wa Sh. 2000 kwa hiyo, kwa mimi umenisaidia kubana matumizi na kuongeza faida," anasema.

Wakati Halima Rashid anausifia kuwa licha ya kudumu kwa muda mrefu hauachi masizi meusi kwenye sufuria hivyo kuwaondolea usumbufu wa kusugua masufuria huku pia bei yake ikiwa ni nafuu hasa kwa familia zenye uwezo mdogo.

Felister Mwalongo, Mratibu wa Programu wa asasi Associazione Mazingira, anasema walitoa mafunzo ya kutengeneza mkaa huo kwa kikundi hicho ikiwa ni utekelezaji wa program za uhifadhi wa hifadhi ya milima ya Udzwangwa na Ushoroba wa Nyerere Selous- Udzungwa.

Alisema pia wamefundisha wakazi wa vijiji vinavyozunguka hifadhi hiyo ikiwamo Mang'ula A, Sole, na Kanyeja namna ya kutengeneza na kutumia majiko ya udongo yaliyoboreshwa ambayo yanatumia vipande vichache vya kuni na jumla ya kaya 52 zinatumia majiko hayo.

Anasema Shirika la Maendeleo ya Kimataifa la Marekani (USAID) kupitia mradi wa Tuhifadhi Maliasili inafadhili utoaji elimu ya uhifadhi wa mazingira katika vijiji vinavyozunguka eneo la Milima ya Udzungwa na njia hiyo.

Kupitia mradi huo, wametoa elimu ya mazingira kwa wanafunzi wa shule za msingi, huku wanafunzi 300 na walimu 45 wakiwa wamefikiwa hadi sasa, na miche 60,000 ya miti ilisambazwa kwa jamii kwa kipindi cha miezi minne.

Kelvin Shirima, Ofisa Mradi wa MJUMITA anaisema hatua mbalimbali zilizotekelezwa kwa msaada wa mradi wa USAID Tuhifadhi Maliasili zimeweza kusaidia kwa kiasi kikubwa kufanya masuala ya uhifadhi wa mazingira kuwa sehemu ya ajenda za mikutano ya kijiji.

Anafafanua, wamekuwa wakifanya kazi na vikundi mbalimbali vinavyojihusisha na uhifadhi wa mazingira katika kanda sita, mikoa 14, wilaya 32 na vijiji 452 nchi nzima.

"Tumekuwa tukifanya kazi na vikundi kuongeza thamani ya bidhaa katika mnyororo wa thamani wa misitu. Lengo letu ni kuhakikisha wakazi wa vijiji wanatambua faida za misitu na kushiriki katika ulinzi wake," alisema Shirima,

Pia, hadi sasa wanafanya ufuatiliaji wa vijiji ili kuhakikisha utawala bora katika utekelezaji wa miradi inayohusiana na misitu na mazingira ambayo inachangia urejeshaji wa njia ya Nyerere Selous-Udzungwa.

Ziara ya JET ilikuwa sehemu ya shughuli chini ya mradi wa USAID Tuhifadhi Maliasili wa miaka mitano (2021 - 2026) unaolenga kuhifadhi bayoanuai ya nchi, kuboresha uunganisho wa makazi na kusaidia maisha ya jamii

AFYA

SAMIA ALIVYODHAMIRIA AFYA TAIFA ...

# Amwaga mabilioni ya vituo afya 1061 na kambi uzazi hospitalini, magari wagonjwa

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI sasa nchini kunatajwa Sera ya Afya ya Mwaka 2007, inaimarishwa kuboresha huduma za afya nchini.

Sura ya maboresho hayo, ambayo ni sehemu ya malengo ya kiserikali hivi sasa, ni kuimarisha huduma za kibingwa na ubingwa, ili kupunguza rufani za wagonjwa nje ya nchi na kuvutia wagonjwa kutoka nje ya nchi.

Vilevile, sera hiyo ambayo sehemu ya Dira ya Maendeleo Awamu ya Sita, kunalengwa kuimarishwa mifumo ya kugharamia afya kila mwananchi anakuwa katika mfumo wa bima ya afya; kuimarisha huduma za kinga na tiba za kukabiliana na magonjwa ya kuambukiza na yasiyoambukiza; pamoja na huduma za uzazi, mama na mtoto.

Katika kurejea maono hayo ya kiafya nchini, ni maudhui ya maelekezo ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, akilenga katika uwekezaji mkubwa kwenye sekta ya afya, lengo kuimarisha ubora wa huduma wa afya kwa wote.



Mwonekano wa upande mmoja wa jengo jipya la upanuzi wa Hospitali ya Meta jijini Mbeya, likiwa na vyumba 223, vikiwamo vitatu vya upasuaji na huduma za dharura wakati ikijengwa **PICHA: MTANDAO.**

### SURA ILIKOFIKA 2024

Hadi kufikia Machi 2024, ufafanuzi wa Wizara ya Afya umekijikita katika maeneo kadhaa, Rais Dk Samia akilenga kuguswe mustakabali wa mambok kadhaa:

Inaanza na , kujenga miundombinu ya kutoa huduma za afya nchini, upatikanaji bidhaa za afya, ubingwa bobezi; uchunguzi wa mionzi; huduma za Afya ya Uzazi wa Mtoto, Magonjwa ya

Pia, kuna suala la magonjwa ya mlipuko; ajira kwa watumishi na udahili wa wanafunzi; Upatikanaji wa Watoa Huduma Ngazi ya Jamii (CHWs); na Sheria ya Bima ya Afya Kwa Wote.

Aidha, Wizara ya Afya inaelekeza kwa Mwaka wa Fedha 2024/25, suala la ujenzi wa miundombinu ya kutoa huduma ya afya nchini, katika Serikali ya Awamu ya Sita, kumeshafanyika uwekezaji mkubwa katika miundombinu ya kutoa huduma za afya.

Eneo mojawapo ni kuwapo vituo vya kutoa huduma za afya katika Serikali ya Awamu ya Sita, kumeongezeka kutoka 8,549 mwaka 2021 hadi kufikia 9,610 Machi 2024; ikiwa ni ongezeko la vituo 1,061.

Sambamba na hilo, inafafanuliwa katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita, kumefanyika uwekezaji mkubwa wa miundombinu ya kutoa huduma za afya, vikiongezeka kutoka vituo 8,549 mwaka 2021 kufikia vituo 9,610 Machi 2024.

Hapo ni sawa na ongezeko la vituo 1,061, inayojumuisha zahanati; vituo vya afya; hospitali zenye hadhi za wilaya na rufani ngazi ya mkoa na kanda; hospitali maalum na taifa.

### UWEKEZAJI MKUBWA UZAZI

Eneo lingine linatajwa kujumuisha suala la kuimarisha huduma za Afya, Uzazi, Mama na Mtoto unaochukua nafasi katika sura ya uwekezaji mkubwa wa mfano, unaojumuisha: Kukamilishwa ujenzi wa jengo la kutoa huduma za afya ya Mama na Mtoto - Hospitali ya Meta, iliyopo jijini Mbeya kwa thamani shilingi 13.2.

Lingine linatajwa ni uendelezaji wa majengo ya huduma za Mama na Mtoto kwenye Hospitali za Rufani Sekou Toure jijini Mwanza; pia miradi mikubwa katika hospitali za Geita, Simiyu, Mawenzi (Moshi), Njombe na Songwe, zikigharimu shilingi bilioni 71.1.

### UPATIKANAJI HUDUMA

Taarifa ya Wizara ya Afya, inafafanua kumeimarishwa sasa upatikanaji wa bidhaa za Afya ya Uzazi, Mama na Mtoto ndani ya miaka mitatu sasa, ikipatikana katika vituo vinavyomilikiwa na serikali, umeongezeka kutoka asilimia 82.5 mwaka 2021 hadi asilimia 88.2 mwaka 2023.

Lingine ni suala la kuimarishwa huduma za saratani ya mlango wa kizazi, kukiwapo jumla ya mashine 140 za uchunguzi wa saratani zimenunuliwa na kusambazwa kwenye vituo 140, vya kutoa huduma za afya katika

Halmashauri 104, ndani ya mikoa 26, jumla ya vikiwa na thamani ya shilingi bilioni 1.1.

### UPASUAJI WAJAWAZITO

Eneo lingine katika orodha hiyo ndani ya Serikali ya Awamu ya Sita, ni kwamba kumeimarishwa huduma za upasuaji wajawazito kwa kuongeza vituo vyenye uwezo kwenye huduma za upasuaji wadharura, kumtoa mtoto tumboni kutoka vituo 340 kitaifa vya mwaka 2021 hadi kufikia 523 mwaka 2023.

Mustakabali mwingine ni kuanzishwa wodi maalum kwa ajili ya kuhudumia za watoto wachanga wagonjwa, hadi kufika Disemba mwaka jana, zilikuwa jumla ya hospitali 189 zinazohudumia, ikilinganishwa na 165 mwaka 2022 na mwaka 2018, zilikuwapo 14 pekee.

Hapo kukaendana na kuimarishwa upatikanaji bidhaa za afya ya uzazi, mama na mtoto katika vituo vinavyomilikiwa na serikali, umeongezeka kutoka asilimia 82.5 mwaka 2021 hadi asilimia 88.2 mwaka 2023.

### SARATANI MLANGO KIZAZI

Ripoti hiyo ya kiserikali inafafanua kwamba, kumeimarishwa huduma za saratani ya mlango wa kizazi, kwa kuwapo mashine 140 za uchunguzi wake, zikinunuliwa na kusambazwa kwenye vituo 140 vya kutolea huduma za afya katika Halmashauri 104 ndani ya mikoa 26. Jmla ya vufa hivyo vina thamani ya shilingi bilioni 1.1

### MFUMO M-MAMA

Mfumo wa huduma za dharura wa kieletroniki unaoitwa kitaalamu 'M-mama', unaoratibu rufani, kwa kusafirisha kinamama wajawazito na watoto wachanga wanaohitaji huduma za dharura, inafafanuliwa Serikali ya Awamu ya Sita, imeshauanzisha hadi kwenye vituo vya afya inatajwa kati ya mwaka 2022 hadi mwaka 2023, mfumo huu umeendelea kufanya kazi katika mikoa yote 31 Tanzania Bara na Zanzibar, kukiwapo mageuzi makubwa ya kuhudumia Watoto wachanga. .

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, akiwa katika wodi maalum ya kuhudumia watoto wachanga wagonjwa katika Hospitali ya Rufani Mount Meru Mkoani Arusha, akashuhudia mfumo huo unavyorahisisha utoaji wa huduma za dharura kwa wakati.

### KUJIFUNGULIA HOSPITALINI

Kuna suala la kuongezeka wajawazito waliojifungulia kwenye vituo vya afya kutoa huduma za afya, nchini, idai imeongezeka maradufu, kutoka asilimia 63 mwaka 2021 hadi asilimia 85 mwaka jana.

"Lengo la nchi ni kufikia asilimia 95 ya wanaojifungulia kwenye vituo vya kutolea huduma za afya ifikapo mwaka 2030," inafafanua taarifa yua Wizara.

### MAGARI YA WAGONJWA

Suala la kuwapo magari ya kubebea wagonjwa yanunuliwa na kusambazwa kila kona na Rais Dk. Samia, ameshakabidhi jumla yao 216, kwa ajili ya kurahisisha utoaji matibabu ya dharura.

Hiyo imeendana na serikali kununua jumla ya magari ya kubebea wagonjwa 727, yakienda kusaidia usafirishaji wagonjwa, wakiwamo kinamama wenye changamoto za uzazi kwa haraka na kuwafikisha katika huduma za rufani, hivyo kupunguza adha kwa wananchi, sambamba na kuepuka vifo vinavyozuilika.

AFYA

# Kilichoko kwenye thamani ya kliniki katika maisha kila siku

**Na Tuntule Swebe na Joyce Lameck**

JE wajua madhara ya kutokuhudhuria kliniki? Kuna kinamama wengi hawajatambua umuhimu wa kuwahi, hata madhara yanayoambatana nayo.

Kuna changamoto za kuchelelewa, zinawakumba kinamama hao. Hapo kuna kasoro za kushindwa kutambua aina ya kundi na wingi wa damu, shinikizo la damu na kuwapo kwa magojwa ya zinaa.

Majumuisho ya ishara mbaya zinazopatikana humo, ndio yanamshurutisha mjamzito kuwahi kliniki, kwani mama, mjamzito anapowahi kliniki na kupewa vipimo pindi anapogundulika, hata kufahamika amepata maambukizi, hupatiwa kinga zinazoweza kumkinga mtoto asipate maambukizi.

Kitaalamu, mtoto anapochelewa kuanza kliniki na kutokufanyiwa uchunguzi, anaingia hatarini kuambukizwa mtoto virusi vya UKIMWI. Hiyo, ni hata kwa mama mwenye presha anapochelewa kuanza kliniki mapema, anakuwa hatarini kupoteza mtoto wake.

Kwake mjamzito, ana kiwango maalum cha presha yake, hivyo anapohudhuria kliniki, wauguzi na madaktari hutambua namna ya kulinda kiwango cha presha yake kiweze kuwa sawa.

Pia, mjamzito mwenye kiwango kidogo cha damu anapowahi kliniki hupatiwa dawa za kuweza kuongeza damu na kupewa ushauri wa kuzikatia aina ya vyakula, anapochelewa kuanza kliniki, anakuwa hatarini kupoteza damu wakati wa kujifungua.

Vilevile inatajwa, mama mwenye kundi la damu 'O', anapochelewa kuanza kliniki, anakuwa hatarini kiafya, anatakiwa kuanza kliniki mapema

KWA kawaida makundi ya damu kwa binadamu yapo manne; A, B, AB na O. Pia, yamegawanyika katika sehemu kuu mbili ziitwazo 'rhesus factors' au inatamkwa 'rizasi fakta'. Rizasi fakta hizi zipo za aina mbili ambazo ni hasi na chanya.

Mama anapokuwa na'rizasi hasi' na baba atakuwa 'rizasi chanya', basi mtoto akiwa tumboni ni lazima arithi kundi la baba na atakuwa na 'rizasi Chanya.'

Damu ya mtoto inaweza kupenya kwenda kwa mama wakati kwa mtoto itapenya kwenda kwa mama wakati wa ujauzito, itapita kwenye kondo la nyuma 'placenta'. Wakati wa kujifungua damu ya mtoto inaweza kujipenyeza katika mishipa midogo.



Baba na mama wakiwa kliniki, mkoani Arusha. **PICHA: MTANDAO.**

Damu ya mtoto inaweza kupenya kwenda kwa mama wakati akiwa tumboni au wakati wa kuzaliwa, hata kusababisha madhara kwa mtoto. Inaelezwa kitaalamu; damu ya mtoto itapenya kwenda kwa mama wakati wa ujauzito, itapita kwenye kondo la nyuma 'placenta'. Wakati wa kujifungua damu ya mtoto inaweza kujipenyeza katika mishipa midogo.

Damu ya mtoto ambayo ni 'rizasi chanya' inapoingia kwa mama, humsababishkia atengeneze kinga ya mwili. Hata hivyo, mwingiliano wa damu unaogusa maisha ya mtoto, husababisha madhara kwa mtoto, ambayo kitaalam huitwa 'Hemolytic Disease of the new Born'.

Ni ugonjwa unaoambatana na kinachoitwa 'hydrops foetalis' ambayo mtoto akiwa tumboni mwa mama, huvimba au hujaa maji (Oedematous), hata anapoteza maisha tumboni au anazaliwa yu njiti.

Kuna hali inayoambatana na kuzaliwa wa manjano, kutokana na chembe nyingi nyekundu za damu kuharibiwa na kinga za mama.

Mtoto anapata upungufu mkubwa wa damu, siku chache baada ya kuzaliwa. Mtoto mwenye umri mdogo anapochelewa kuanza kliniki, maisha yake yanaangukia hatarini, kwani nyonga zake zinakuwa hazijatanuka kiasi cha kumudu mabadiliko ya uzazi, hata kuchangia kifo chake.

Mtoto anapowahi kliniki na kupewa msaada wa kitabibu, ni dhahiri maisha yake yanaweza kuokolewa kwa kufanyiwa operesheni, kinyume chake ni hatari kiafya hata kupoteza maisha.

**KUTOKA WIZARANI**

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, anaelekeza, kuondolewa vikwazo vya mjamzito, pindi anapoenda kliniki, bila ya mwenza wake.

Ilikuwa Novemba 30, 2023 kwenye Maadhimisho ya Siku 16 Kupinga Ukatili wa Kijinsia, yaliyofanyika wilayani Muheza, mkoani Tanga, akiwa na ufafanuzi:

"Tusiweke vikwazo kwa wanawake ambao wamepata ujauzito na wanaenda kliniki bila ya wenza wao kupata huduma. Tuwashauri na tuwape elimu waende na wake zao, lakini tusiwanyime huduma, kwa sababu hawakwenda na wenza wao.

"Hii 'imepelekea' wanawake wanatafuta bodaboda au mwanaume yeyote ampeleke kliniki ili apate huduma hii haikubaliki."

Anashauri wanaume wahamasishwe na kupewa umuhimu wa baba na mama wanapoenda pamoja kliniki, huku kukiwapo maoni ya ziada ya umma, kwamba mjamzito mwenye kiwango kidogo cha damu, anapowahi kliniki apatiwe dawa kuongeza damu na apewe ushauri wa mlo sahihi.

Pia, inaendana tahadhari kwamba, majamzito huyo anapochelewa kuanza huduja za kliniki, anakuwa hatarini kupoteza damu nyingi wakati wa kujifungua, akihatarisha maisha yake.

Vilevile inatajwa mama mwenye kundi la damu O, anapochelewa kuanza kliniki anakuwa hatarini kumpoteza kwani anapoanza kliniki mapema.

• ***Makala hii inatokana na mabadiliko mbalimbali katika mwenendo wa afya ya umma.***

## Anavyoishi anayepoteza kumbukumbu na elimu kutoka bingwa anayemtibu

**Inatoka Uk. 11**

Wataalam hufanya usaili unaomhusisha mteja, familia na watu wengine wanaomzunguka kama itahitajika kufanya hivyo. Mtaalam pia hufanya vipimo mbalimbali vikiwamo vya damu, nyurosaikolojia (Neuropsycholological assessments), pamoja na vipimo vya CT Scan au MRI kusaidia kubaini chanzo cha kupoteza kumbukumbu.

Shinikizo la juu la damu (Hypertension) likitibiwa vizuri inapunguza uwezekano wa kupoteza kumbukumbu kwa kiasi kikubwa.

Mgonjwa anayetumia dawa za shinikizo la juu la damu, anapopata tatizo kupoteza kumbukumbu ni lazima uchunguzi ufanyike kubaini chanzo," anasema bingwa huyo.

**CAG ADOKEZA**

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG), iliyotolewa Machi mwaka huu, ilibaini kunahitajika maboresho zaidi katika utoaji wa huduma bora za afya ya akili nchini.

Ilisema, watu wenye matatizo ya akili katika ngazi ya jamii na badala yake ulilenga watumiaji wa dawa za kulevya, wazee, watu wenye ulemavu, watoto walio katika mazingira magumu na waliopata mimba za utotoni.

Kwamba hali hiyo, ilichangiwa na ukosefu wa fedha za kutosha kwa ajili ya huduma za ustawi wa jamii na kukosekana kwa maofisa ustawi wa jamii katika ngazi za chini, vikiwamo vijiji na mitaa.

Ilisema, imebaini rasilimali zisizotosheleza (wataalamu, miundombinu, vifaatiba, na dawa) na kutopatikana kwa huduma za utengamo katika vituo vya kutolea huduma hizo.

Pia, CAG alibaini kulikuwa na ukosefu wa huduma za utengamo kwa ajili ya kuendeleza ujuzi, ushirikiano wa jamii, na misaada inayozingatia urejeshaji, na kwamba kati ya mikoa 28, ni mitano ndiyo ilikuwa na vituo vya utengamo kwa ajili ya huduma za afya ya akili.

Mikoa hiyo ni Kilimanjaro, Mwanza, Dar es Salaam, Dodoma, na Kigoma.

**BAJETI YATENGWA**

Mei mwaka huu, bungeni Dodoma, kwa mara ya kwanza, serikali ilitenga bajeti ya Sh. bilioni 9.1 kwa ajili ya afya ya akili.

Pia serikali ilitangaza kuanzishwa mtaala wa Stashahada ya Juu ya Afya ya Akili kwa Wauguzi, ambayo itaanza kudahili wanafunzi wa mwaka wa masomo 2024/2025.

Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Wataalamu wa Afya ya Akili (MEHATA, Bingwa Mwandamizi wa Afya na Magonjwa ya Akili kutoka Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. Saidi Kuganda, anasema;

Fedha hizo zinakwenda kuimarisha huduma ya afya, elimu, kuongeza wataalamu na matibabu kwa wenye matatizo ya akili, kuongeza idadi ya kuwafikia wanaougua.

"Napongeza serikali kwa mara ya kwanza kuelekeza kabisa fedha kwa ajili ya eneo hili, ...itaongeza wigo wa huduma kwa wanaougua, kutoa elimu kwa umma.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, akiwasilisha bajeti ya wizara hiyo, akiwa bungeni, anasema katika mwaka wa fedha 2024/2025, zimetengwa shilingi 9,318,528,988 kwa ajili ya afya ya akili.

Anasema katika vipaumbele 10 vya wizara kwenye bajeti hiyo, kipo mahsusi kwa ajili ya afya ya akili, kwa lengo la kuimarisha huduma za utengamo kwa watoto, wazee, watu wenye ulemavu.





# Halmashauri ya Ikungi yang'ara ukaguzi wa CAG

**Na Thobias Mwanakatwe,**

IKUNGI

HALMASHAURI ya Wilaya ya Ikungi mkoani Singida katika kipindi cha miaka 10 imezidi kung'ara baada ya kupata hati safi mfululizo, kuanzia mwaka wa fedha 2013/2014 hadi 2022/2023.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya wilaya hiyo, Justine Kijazi, alisema hayo jana wakati wa kikao maalum cha baraza la madiwani cha kujadili majibu ya hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Alisema kulingana na taarifa ya CAG ya kuishia Juni 2023, Halmashauri ya Ikungi ilikuwa na hoja tano, hoja za miaka ya nyuma ni 24 na hoja za mwaka 2022/2023 ni hoja 28.

Kijazi alisema hoja 30 zilifungwa na kubaki ni hoja 22 ambazo ziko kwenye hatua mbalimbali za utekelezaji.

"Tunashukru sana ofisi ya mkaguzi wa ndani ambayo ni jicho la halmashauri kusimamia hoja, sasa tunajiandaa na ukaguzi wa mwaka 2023/2024, tuendelee kuomba ushirikiano ili halmashauri iendelee kupata hati safi, tutaendelea kufanya kazi kwa kufuata sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya serikali," alisema.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, amesema ni jambo kubwa na la kupongezwa na kutia moyo kwa halmashauri kupata hati safi kwa mfululizo wa miaka 10.

Alisema wakaguzi wa ndani ni walimu wazuri sana ambao kama halmashauri inazingatia ushauri wao, haiwezi kuwa na hoja nyingi za ukaguzi.

"Katika halmashauri ukiona hoja zinajitokeza ujue kuna mtu amekula bila kunawa, naagiza kila mzalisha hoja iwe ni idara abanwe," alisema Dendego.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, Ally Mwanga, aliema halmashauri hiyo kupata hati safi mfululizo kwa miaka 10 ni kutokana na ushirikiano uliopo wa watendaji na madiwani.

Akizungumza kuhusu hoja za CAG, alisema kimsingi hakuna halmashauri inayofurahia kuwa na wingi wa hoja, hivyo jukumu la kila mmoja kuhakikisha hawazalishi hoja mpya.

Naye Katibu Tawala Mkoa wa Singida, Dk.Fatuma Mganga, alisema kila halmashauri iweka mkakati madhubuti kujibu hoja za CAG ambapo kila halmashauri ziwe zaidi ya tisa.

Dk.Mganga alisema moja ya vigezo vya kupima utendaji wa halmashauri ni uwingi wa hoja, hivyo kinachotakiwa ni kuongeza jitihada kuhakikisha hoja zilizopo zinajibiwa na kutozalisha nyingine.

Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, Thomas Apson alisema halmashauri hiyo inastahili pongezi kwa kupata hati safi mfululizo kwa miaka 10.

Aidha, Apson alisema halmashauri iongeze ubunifu kwa kuwa na vyanzo vipya vya mapato badala ya kila mwaka kuwa na vyanzo vile vile na kutolea mfano majimoto kwamba kinaweza kuwa chanzo kizuri cha mapato.

## Wabuni mifumo kuzuia udanganyifu wa mitihani

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WANAFUNZI wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) wamebuni mifumo mbalimbali ambayo itasaidia kupunguza uvujaji na udanganyifu katika mitihani.

Mifumo hiyo pia itasaidia kupunguza changamoto za uchaguzi wa kozi za vyuo na vyuo vikuu kwa kutumia teknolojia ya akili mnemba.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti wakati wa kufunga Wiki ya Tafiti na Uvumbuzi katika ya Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu ya UDOM, wanafunzi waliobuni mifumo hiyo walisema uvumbuzi wao umetokana na uwepo wa kero nyingi katika mnyororo wa mitihani ya chuo pamoja na mchakato wa maombi ya kozi.

Mmoja wa wanachuo hao, Irene Mawena alisema mifumo hiyo inakwenda kusaidia kutatua changamoto hizo ambazo hutokea mara kwa mara wakati wa kipindi cha mitihani.

Makamu Mkuu wa UDOM, Profesa Lughano Kusiluka, aliwataka vijana hao kuendelea kutumia vyema uwezo wao wa kufanya utafiti na bunifu ili zisaidie kutatua changamoto mbalimbali kwa jamii na wao wenyewe ziwasaidie kujikwamua kimaisha.

Alisema hakuna sababu ya vijana kurandaranda mtaani badala yake watumie taaluma yao kujiajiri ili wajikwamue kiuchumi wao na familia zao.

Alisema wanapaswa kutumia utafiti walizofanya pamoja na ubunifu mbalimbali kutengeneza mifumo ambayo wataisambaza kwa jamii.

Akizungumzia kuhusu mifumo ya kuzuia uvujaji wa mitihani, alisema itasaidia kupunguza adha hiyo kwa wanafunzi inapofika kipindi cha mitihani.

Alisema wiki ya ubunifu imeleta matokeo chanya, kwamba wanafunzi wameonyesha ubunifu wa pamoja na kusaidia wananchi katika masuala ya teknolojia.




Mkuu wa Kitengo cha Usafi na Udhibiti wa Takangumu cha Jiji la Dodoma, Dickson Kimaro, akizungumza na wafanyabiashara wa soko la wazi la Machinga na waathirika wa dawa za kulevya wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Kupinga Dawa za Kulevya jijini humo jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Kliniki ya msaada kisheria kwa wananchi yazinduliwa

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MWANASHERIA Mkuu wa Serikali (AG), Jaji Dk. Eliezer Feleshi, amezindua kliniki ya msaada na elimu ya kisheria kwa umma inayokusudia kusogeza huduma za sheria karibu na wananchi.

Hatua hiyo ni utekelezaji wa maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Akizindua kliniki hiyo jana jijini hapa, Jaji Dk. Feleshi alisema pamoja na kufikisha huduma za sheria karibu na wananchi pia itasaidia kufikia malengo ya kupunguza migogoro dhidi ya serikali.

"Kwani wananchi wakisikilizwa na kupata suluhu ya changamoto zao za kisheria dhidi ya serikali hawatakuwa na haja ya kuishtaki serikali katika vyombo mbalimbali vya utatuzi wa migogoro ya nje na ndani ya nchi," alisema Jaji Feleshi.

Aidha, alisema lengo la kliniki hiyo ni kutekeleza maagizo ya Rais Samia, ambayo amekuwa akiyatoa mara kwa mara kwa viongozi wa serikali kuweka utaratibu wa kusikiliza malalamiko ya wananchi na kuyatatua.

"Ikiwa ni pamoja na kuwaongoza katika taratibu za kupata haki zao pale zinapovunjwa au zinapoonekana kuelekea kuvunjwa na kudumisha utawala bora kwa kuimarisha utulivu wa sheria nchini," alisema.

Kadhalika, alisema kusogeza huduma za sheria karibu na wananchi kutasaidia kuongeza utengamano na utulivu katika jamii na kuchochea maendeleo kwa jamii na taifa kwa ujumla.

"Nchi yetu hivi sasa tunahitaji sana wawekezaji hivyo kama hakutakuwa na utengamano na utulivu, wageni hawezi kuja kuwekeza nchini kutokana na migogoro itakayokuwapo hivyo kliniki hii itasaidia kuboresha mazingira na kuongeza imani kwa wawekezaji wa ndani na nje," alisema.

Vile vile, alitoa rai kwa mawakili wote wa serikali kutenga muda na kuwasikiliza wananchi katika maeneo yao kupitia kamati za ushauri wa kisheria ngazi za mikoa na wilaya zilizozinduliwa na Waziri Mkuu Kassim Majaliwa.

"Aidha, nitumie fursa hii kuwakumbusha wakuu wa mikoa na wilaya wote nchini ambao bado hawajakamilisha kuteua wajumbe wawili wa kamati hizo kwa mujibu wa mwongozo wa huduma za ushauri wa kisheria ngazi za mikoa na wilaya kufanya hivyo ili kamati zianze kufanya kazi ya kusikiliza malalamiko ya wananchi," alisema.

Naye Makamu wa Rais wa Chama cha Mawakili wa Serikali Tanzania, Ellen Rwijage, alitoa wito kwa Watanzania wote wenye kero zinazohusu masuala ya sheria kujitokeza kupata huduma hiyo bure.

Hata hivyo, alisema mawakili wa serikali wamejipanga kutoa huduma kwa muda wa wiki moja ambao utatumika kusikiliza na kutoa elimu na ushauri wa kisheria.





# Viongozi wakwamisha ujenzi shule

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

VIONGOZI wa serikali na wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tawi la Mtaa wa Kikula Halmashauri ya Mji Makambako mkoani Njombe, wametakiwa kumaliza tofauti zao za kisiasa ili kuhakikisha eneo la ujenzi wa shule mpya ya msingi linapatikana.

Wananchi wa mtaa huo walitoa kauli hiyo baada ya Katibu wa CCM wa tawi hilo na aliyekuwa mjumbe wa serikali ya mtaa huo kumtuhumu Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa na wajumbe wake kuwa wameuza ardhi yenye ukubwa wa ekari nane kwa Sh. milioni 11.

Inadaiwa kuwa hali hiyo imesababisha kushindwa kulipa fidia eneo lingine lenye ukubwa wa ekari 4.6 kwa madai ya kwamba fedha iliyopo haitoshi.

Wakizungumza katika mkutano ambao umefanyika ofisi ya Mtaa wa Kikula wananchi hao akiwemo Yuda Longolela alisema changamoto kubwa iliyopo katika mtaa wao ni mgogoro wa kisiasa uliopo kwa baadhi ya viongozi wa serikali na wale wa chama tawala.

"Tunaomba kuundwa kwa kamati ili kufanikisha upatikanaji wa eneo la ujenzi wa shule ya msingi ambayo itasaidia kupunguza utoro kwa wanafunzi wanaosoma Shule ya Msingi Juhudi iliyopo Kipagamo," alisema Longolela.

Naye Inoncensia Mtenda alisema mgogoro huo unasababishwa na viongozi kubishana, hivyo wanaomba kumaliza changamoto hiyo ili kuweza kupata eneo ili shule iweze kujengwa.

Aidha, Katibu wa CCM tawi la Kikula, Tadei Mhongole alisema licha ya ekari nane kuuzwa pia mwenyekiti wa mtaa kwa kushirikiana na wajumbe wake walitaka kuuza eneo la ofisi ya serikali ya mtaa huo hali ambayo ilimlazimu kuiandikia barua kamati ya siasa ya kata ili kuzuia eneo hili lisiuzwe.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Kikula, Batwery Makweata, alisema walitaka kuuza eneo hilo na wajumbe kutokana na CCM tawi hilo kuzuia wasikusanye michango kwa wananchi Sh. 30,000 ambacho walikuwa wanachangia.

Alisema fedha walizouza hekari nane hazitatosha kununua eneo lingine kutokana na eneo wanalotaka kununua kufanyiwa uthamini upya na wataalamu wa halmashauri.

Diwani wa Kata ya Makambako, John Ngimbuchi aliunda kamati ambayo itahusika na kutafuta eneo kwa ajili ya ujenzi wa shule ya msingi mpya.



Ofisa Kilimo wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Gideon Mapunda (kulia), akizungumza na viongozi wa vyama vya ushirika vya wakulima wa kahawa wa halmashauri hiyo, juzi alipokuwa akifungua mafunzo ya kuwajengea uwezo wa usimamizi wa vyama hivyo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Dk. Tulia atoa msaada miche maparachichi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WANANCHI zaidi ya 350 kutoka kata za Mwansekwa, Itagano na Nsalaga katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya, wamepatiwa miche ya maparachichi kwa lengo la kuipanda kwenye maeneo yao ili kujiongezea kipato na kutunza mazingira.

Miche hiyo imegawiwa kwa wananchi hao na Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson kupitia taasisi yake ya Tulia Trust ambayo inajishughulisha na mambo mbalimbali ya kijamii ikiwemo uwezeshaji wa wananchi kiuchumi.

Akizungumza wakati wa kukabidhi miche hiyo, Ofisa Habari wa taasisi hiyo, Ahadi Kalinjila alisema Dk. Tulia aliamua kugawa miche hiyo kwa wananchi ili kuwasaidia kujiwekea mazingira ya kujiinua kiuchumi.

Alisema maparachichi ni moja ya matunda ambayo yana soko zuri la ndani na nje ya nchi na hivyo wananchi wakiitunza vizuri watakuwa na nafasi ya kujiinua kiuchumi na kuyatumia matunda hayo kama chakula na hivyo kukabiliana na matatizo ya lishe.

Alisema waligawa miche 150 kwa wananchi wa Kata ya Mwansekwa, miche 150 kwa wananchi wa Kata ya Itagano na miche 50 kwa wananchi wa Kata ya Nsalaga na kwamba wanaendelea kufuatilia ili kuona maeneo mengine ambayo matunda hayo yanastawi ili waendelee kusambaza.

"Serikali imeweka mazingira rafiki ya kuuza matunda haya nje ya nchi na hata ndani ya nchi, kwahiyo tuna uhakika kwamba mbali na kutunza mazingira lakini wananchi hawa wakiitunza vizuri watajipatia kipato yatakapoanza kuzaa," alisema Kalinjila.

Alisema kwa sasa matunda ya maparachichi yana soko zuri hata ndani ya mkoa huo wa Mbeya kwa maelezo kuwa kuna baadhi ya wawekezaji wameanza kuchakata zao hilo na kuzalisha bidhaa mbalimbali ikiwemo mafuta ya kupikia.

Baadhi ya wananchi walionufaika kwa kupata miti hiyo walimshukuru Dk. Tulia kwa msaada huo wakidai kuwa utawasaidia kuboresha maisha yao huku wakiahidi kuitunza na kuhakikisha inakua.

Mwenyekiti wa Mtaa wa Mengo Kata ya Mwansekwa, Elias Mwaweya alisema matunda hayo ni muhimu kwa afya za wananchi na hivyo watahakikisha wanasimamia ili miti hiyo ikuwe na kuwasaidia wananchi.

Alisema itawasaidia pia wananchi kupunguza gharama za kwenda kununua matunda hayo kwa maelezo kuwa watakuwa wanachuma kwenye miti yao na kutumia kama chakula.

"Ukienda sokoni kununua maparachichi gharama yake huwa siyo ndogo, sasa tumeshapatiwa miti hii na nina imani kuwa kwa aina ya ardhi ya maeneo yetu miti hii itakua na tutakula kwa muda mrefu maana hii miti inawahi kuanza kuzaa na inachelewa kuzeeka," alisema Mwaweya.

Diwani wa Kata ya Itagano, Yuda Mbalamwezi alisema kata yake ni miongoni mwa maeneo ya Jiji la Mbeya ambayo miti ya maparachich inastawi na kwamba wananchi walishaanza kuzalisha na hivyo wameongezewa nguvu.

Alisema Dk. Tulia amekuwa akionyesha upendo kwa wananchi wa kata hiyo kwa maelezo kuwa kabla ya kuwapelekea miche hiyo alishawapelekea matangi kwa ajili ya kuhifadhia maji kwenye kituo cha afya cha kata hiyo.

Alisema vilevile walipatiwa madawati na mifuko ya saruji kwa ajili ya Shule ya Sekondari ya Itagano pamoja na kuchangia ujenzi wa ofisi ya kata hiyo.

# CCM yaingilia mgogoro halmashauri na wakulima

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Mbeya kimeingilia kati mgogoro wa ushuru wa mazao unaoendelea kufukuta kati ya Halmashauri ya Wilaya ya Mbarali na wakulima wa mpunga, ambao wanalalamikia kutozwa ushuru zaidi ya mara mbili.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Katibu wa Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa CCM Mkoa wa Mbeya, Christopher Uhagile alisema chama hicho kimeagiza viongozi wa halmashauri hiyo wanatakiwa kukutana na wakulima pamoja na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI) ili kutatua mgogoro huo.

Alisema wakulima wamekuwa na malalamiko ya muda mrefu kuhusu utaratibu unaotumika kutozwa ushuru wakidai kuwa unawaumiza, huku halmashauri nayo ikiwa na msimamo wake hali ambayo inasababisha hata hali ya amani kuwa shakani.

Alisema chama hicho baada ya kufuatilia kilibaini kuwa mgogoro unazidi kuichonganisha serikali na wakulima na hivyo ili kuweka sawa jambo hilo inahitajika mazungumzo ya kawaida.

"Chama kimeona ni vizuri mgogoro huu umalizike ili wananchi waendelee kufanya shughuli zao kwa amani na halmashauri iendelee kukusanya mapato kwa utaratibu ambao hautakuwa kero kwa wananchi hao," alisema Uhagile.

Alisema ushuru wa mazao ni muhimu kwa maendeleo ya taifa lakini ni lazima ukusanyaji wake usiwe wa kutumia nguvu na badala yake uwe wa kisheria.



# Serikali kutumia boti kusafirisha wagonjwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Zanzibar imesema serikali imejipanga kutafuta boti za kubebea wagonjwa za kisasa zenye sifa ya kuwasafirisha wagonjwa kutoka katika visiwa vidogo vya Pemba, ili kuwapatia huduma bora na za kisasa.

Hayo yalisemwa jana na Naibu Waziri wa Wizara hiyo, Hassan Khamis Hafidh, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali aliloulizwa na mwakilishi wa Mtambwe Dk. Mohammed Ali Suleiman.

Dk. Mohammed alitaka kujua ni upi mpango wa muda mrefu wa serikali katika kutatua tatizo la afya katika visiwa kama vile Kisiwa cha Kokota.

Alisema serikali kupitia Wizara ya Afya inafahamu usafiri huo wa majini hususani boti za kubebea wagonjwa iliyopo Wete inachangamoto kubwa hasa ya kiwango kikubwa cha mafuta kusafirishia wagonjwa na pia kutokana na mifumo ya boti inahitaji huduma kubwa.

Alisema changamoto hiyo haijasimamisha huduma za kuwasafirisha wagonjwa kwa sababu kuna boti za 'fiber' tofauti ambazo zimeingizwa katika mfumo wa M-MAMA ili kuweza kuendelea kusafirisha wagonjwa na wanapata huduma hiyo.

Alisema Wizara ya Afya inaendelea na juhudi za kuongea na kampuni ya Yamaha ili kuifanyia huduma kuu boti hiyo, ili iendelee kutoa huduma za kusafirisha wajawazito na watoto.

Aidha, alisema sababu kubwa inayosababisha boti hiyo ya Wete ni kuwa na uhitaji mkubwa wa mafuta pia kukosekana kwa huduma na kwa upande wa Kisiwa cha Kojani huduma zinaendelea kutolewa kupitia boti ambazo zipo katika mfumo wa M-MAMA.

Akijibu swali aliloulizwa na mwakilishi wa Wingwi, Kombo Mwinyi Shehe, aliyetaka kujua tangu Wizara ya Afya itoe mikataba ya kazi kwa kampuni mbalimbali ikiwemo lacent NSK pamoja na Self II ni kwa kiasi gani huduma za afya zimeimarika.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri huyo alisema baada ya kuanza kufanya kazi na kampuni binafsi huduma zimeimarika ikiwemo upatanikanaji wa dawa kwa asiliamia 90.

Alisema pia usafiri hospitalini, nidhamu ya kazi imeongezeka, chakula cha wagonjwa kinapatikana kwa wakati, ufuaji wa nguo za wagonjwa pamoja uendeshaji hospitali.

Alisema: "Madaktari bingwa walioongezeka kwa ujio wa kampuni hizi ni sita ambao ni wa magonjwa ya watoto, upasuaji kwa kutumia njia ya matundu, mifupa, huduma za dharura, usingizi na pua, masikio na koo".




Mwandishi wa Gazeti la Nipashe, Zanzibar, Rahma Suleiman (kulia), akizungumza wakati wa mafunzo ya uandishi wa habari wanawake kuhusu matumizi sahihi ya kidijitali yaliyoandaliwa na Taasisi ya Zaina Foundation Tanzania, mjini Unguja juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wanahabari watakiwa kuwa kidijitali kuelekea uchaguzi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Zaina Fondation Tanzania, Zaituni Njovu amesema mbinu za matumizi sahihi ya mtandao na masuala ya kidijitali ni muhimu kwa waandishi wa habari, hasa katika kipindi hiki cha kuelekea Uchaguzi Mkuu.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki visiwani Zanzibar wakati akizungumza na waandishi wa habari baada ya kufungua mafunzo kwa waandishi wa habari wanawake kuhusu matumizi sahihi ya kidijitali yaliotolewa na taasisi hiyo.

Alisema matumizi hayo yatawasaidia kubaki salama na kuelimisha jamii kuepukana na matatizo mbalimbali ya ukatili wa kijinsia mtandaoni.

Alisema waandishi wa habari wanaweza kusaidia kupunguza ukatili wa kijinsia mtandaoni wanaofanyiwa wanawake hususani kipindi cha Uchaguzi Mkuu.

Hivyo, aliwataka waandishi wa habari kuitumia fursa ya kidijitali katika kutuma taarifa zao lakini pia kuandika maudhui ya wanawake ili kuwa salama.

Aidha, alisema kuwa wanawake ndiyo waathirika wakubwa wa udhalilishaji mtandaoni, hivyo ni vyema kutumia majukwaa ya kidijitali katika kukuza demokrasia nchini na kuongeza ushiriki wa wanawake katika Uchaguzi Mkuu.

Hata hivyo, aliwataka wanawake kuacha kuchukua picha na maneno ambayo yenye maudhui ya kujidhalilisha ili kuepukana na udhalilishaji mitandaoni, lakini ikitokea kudhalilishwa wasisite kuripoti katika vyombo vya sheria.

Alisema inapofika kipindi cha uchaguzi wanawake wanapogombea nafasi mbalimbali za uongozi hukumbana na kadhia nyingi za udhalilishaji mitandaoni kwa lengo la kukatishwa tamaa, hivyo aliwataka wanawake kutovunjika moyo.

Baadhi ya waandishi wa habari waliopatiwa mafunzo hayo walisema kuwa watakuwa mabalozi wazuri wa kuielimisha jamii hasa wanawake kuacha kutuma maudhui ya picha, video au maandishi ambayo yatawavunjia heshima na utu wao ili kupukana na udhalilishaji mtandaoni.

# Wizara yajinasibu kutumia mabalozi kuvutia watalii

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Utalii na Mambo ya Kale Zanzibar imesema kuwa inaendelea kutekeleza mipango ya kuvutia masoko mapya zaidi pamoja na kubuni vyanzo vipya vya masoko hayo kwa mabalozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Waziri wa Wizara hiyo, Mudrik Ramadhan Soraga aliyasema hayo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali aliloulizwa na mwakilishi wa Mwanakwerekwe, Ameir Abdallah aliyetaka kujua ni ipi mikakati ya wizara hiyo katika kubuni namna ya kuvuna masoko mapya ya utalii, badala ya kuendelea kuzitegemea nchi walizozizoea.

Akijibu swali hilo, Soraga alisema wizara yake imeendelea kushirikiana na ubalozi wa Tanzania nchini China na Korea, kuyavutia na kuyakodisha masoko mapya.

Aidha, alisema wizara, kwa kutekeleza juhudi na jithada za viongozi wa kitaifa, akiwemo Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi, na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan.

Alisema viongozi hao wameifungua zaidi Tanzania kupitia filamu za The Royal Tour na Amazing Tanzania, imekuwa mstari wa mbele katika kuwaalika watu maarufu, waandishi wa habari, wafanyabiashara kuja Zanzibar na kufikisha ujumbe wa kuitangaza na kuitembelea Zanzibar pindi wakirudi nchini mwao.

"Kwa mfano, hivi karibuni wizara ilishirikiana na shirika kubwa la utangazaji ulimwenguni la CNN kupitia programu yake ya Quest Business Traveller na kuweza kuitangaza Zanzibar kwa watazamaji zaidi ya bilioni mbili duniani na zaidi ya nchi 200 duniani. Hizo zote ni jitihada za makusudi katika kuvutia masoko mapya ya utalii" alisema.

Hata hivyo, alisema dhana ya utalii kwa wote kupitia kamati za utalii za wilaya inaendelea vyema na utekelezaji wake, ambapo wizara imekuwa ikiwashirikisha wananchi wa makundi yote kushiriki kikamilifu kwenye sekta ya utalii.

Alisema makundi hayo yanashirikishwa lengo ni kujiweka karibu na wananchi kupitia makatibu wa kamati hizo ambao ni wafanyakazi wa wizara ambao hupokea changamoto kutoka kwa wananchi na kuzifikisha wizarani kwa ajili ya kupatiwa ufumbuzi husika.

Alisema pia hutekeleza mpango wa wizara unaobeba dhana ya utalii kwa wote kwa kushirikiana na kamati.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**PETER PIUS KALOKOLA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S 4515/0024 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia ST. ACHILEUS KIWANUKA mwaka 2021. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: PHQ/DAR/KIN/545390/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**VEDASTUS AMANDI KIMARIO** anatangaza kupotea kwa pikipiki zenye usajili namba MC 143 AEE na MC 244 AEE kwa yeyote atakaeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: PHQ/DAR/KIN/126282/2024**

## KUPOTEA KWA VYETI



**ERASTO RAPHAERY MLOTI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S1341 – 0068 Kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **NAKAGURU SECONDARY SCHOOL** mwaka 2016, na **VYETI VYA VETA** vyenye usajili namba **10/CBA-11/EL/20M/085** na **10/CBA-111/EL/21M/090** vilivyotolewa mwaka 2020 na 2021. Kwa yeyote atakaeviona atoe taaifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: PHQ/MOR/KIL/6310/2024**

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**IVAN C. CHACHA** anatangaza kupotea kwa result slip ya kidato cha yenye index namba S4439-0118 iliyotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia CENTENNIAL CHRISTIAN SEMINARY SCHOOL mwaka 2023 . kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA:PHQ/DAR/UBU/126802/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**RYAN CHRISTOPHER MTASINGWA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0108/0140/2021 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia IFUNDA TECHNOLOGY SECONDARY SCHOOL mwaka 2021. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: PHQ/DAR.KIN.11878/2024**

## KUPOTEA KWA VYETI



**MICHAEL GOODLUCK URIO** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0782-0139 kilichotolewa Baraza la Mitihani la Taifa kupitia MWIKA HIGH SCHOOL mwaka 2006, cheti cha kidato cha sita chenye index namba S0134/0574 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia MOSHI SECONDARY SCHOOL mwaka 2009 na pia anatangaza kupotea kwa cheti cha chuo Cha BACHELOR OF SCIENCE IN EDUCATION chenye usajili namba T/DEG/09/960 kilichotolewa ST. AUGUSTINE UNIVERSITY mwaka 2012. Kwa yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: PHQ/DAR/UB/126130/2024**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA DODOMA**
**MAHALI DODOMA**
**MAOMBI MADOGO NA. 296 YA MWAKA 2022**
**BAINA YA**
**SHABANI MATANDILA ............ MDAI**
**DHIDI YA**
**HEZEKIA NDAHANI CHIBULUNTE ....... MDAIWA**

**KWA:**
**HEZEKIA NDAHANI CHIBULUNTE**

**POPOTE ULIPO**
**YAH: KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa muombaji ameleta maombi yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala ya maombi ambayo inapatikana katika Baraza hili

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Baraza hili wewe binafsi, Wakili au mwakilishi yeyote ambaye anaruhusiwa kisheria tarehe 01.08.2024 saa 3:00 asubuhi. Kwa ajili ya kutaja.

ANGALIZO: Kama haukuhudhuria tarehe iliyotajwa hapo juu. Baraza likithibitisha kuwa umepokea hati ya wito, Baraza linaweza kutoa hukumu dhidi yako.

Hati hii imetolewa kwa Amri yangu na Lakiri/Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 24 ya mwezi Juni, 2024.

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**IN THE DISTRICT COURT OF KAHAMA**
**AT KAHAMA**
**CIVIL NO CASE 3721/2024**
**REF NO.20240226100003721**
**ESTER DAVID ROBERT............PLAINTIFF**
**DHIDI YA**
**DAVID MBOYA............1ST DEFENDANT**
**ESTER MOSHA.........2ND DEFENDANT**
**EMMANUEL LUCAS..................3RD DEFENDANT**

**KWA: EMMANUEL LUCAS**
**POPOTE ULIPO**

Kwa kuwa Mdai ameleta maombi ya kupeleka wito kwa kutumia gazeti hapa mahakama ya wilaya ya Kahama katika shauri tajwa hapo juu,

Ambapo shauri limepangwa kutajwa tarehe 19/07/2024.

Unaamriwa kuhudhuria mbele ya mahakama hii mnamo tarehe 19/07/2024, saa 02.30 asubuhi bila kukosa au kuchelewa ambapo siku hiyo shauri hili litakuja kwaajili ya kutajwa.

Fahamu kuwa usipohudhuria siku hiyo, shauri hilo laweza kuamriwa kutolewa hukumu upande mmoja bila kuwepo.

Imetolewa kwa AMRI yangu na CHAPA ya mahakama hii leo 18 June 2024.




**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**IN THE DISTRICT COURT OF KAHAMA**
**AT KAHAMA**
**CIVIL NO CASE 3721/2024**
**REF NO.20240226100003721**
**ESTER DAVID ROBERT.........PLAINTIFF**
**DHIDI YA**
**DAVID MBOYA............1ST DEFENDANT**
**ESTER MOSHA.........2ND DEFENDANT**
**EMMANUEL LUCAS.........3RD DEFENDANT**

**KWA: ESTER MOSHA**
**POPOTE ULIPO**

Kwa kuwa Mdai ameleta maombi ya kupeleka wito kwa kutumia gazeti hapa mahakama ya wilaya ya Kahama katika shauri tajwa hapo juu,

Ambapo shauri limepangwa kutajwa tarehe 19/07/2024.

Unaamriwa kuhudhuria mbele ya mahakama hii mnamo tarehe 19/07/2024, saa 02.30 asubuhi bila kukosa au kuchelewa ambapo siku hiyo shauri hili litakuja kwaajili ya kutajwa.

Fahamu kuwa usipohudhuria siku hiyo, shauri hilo laweza kuamriwa kutolewa hukumu upande mmoja bila kuwepo.

Imetolewa kwa AMRI yangu na CHAPA ya mahakama hii leo 18 June 2024.




**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA RUFANI YA TANZANIA**
**INAYOKETI ARUSHA**
**SHAURI LA MAOMBI YA MADAI**
**NA. 186/02 YA 2023**
**HANSPAUL INDUSTRIES LIMITED .....MUOMBAJI**
**DHIDI YA**
**TIB DEVELOPMENT BANK LIMITED & MWENZAKE ........MJIBU MAOMBI**

**KWA:**
**MANAGING DIRECTOR,**
**MOUNT MERU FLOWERS LIMITED,**
**P.O.BOX 285,**
**ARUSHA**

**POPOTE ULIPO**

Unajulishwa kwamba shauri la madai tajwa hapo juu limepangwa kusikilizwa na mahakama hii hapa Arusha tarehe 12 Julai, 2024 saa tatu kamili asubuhi (9:00)

Unapaswa kuhudhuria siku na tarehe iliyopangwa bila kukosana endapo hautahudhuria wewe mwenyewe au mwakilishi wako anayetambulika kisheria basi maombi haya yatasikilizwa bila ya uwepo wako.

Imetolewa lwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 21 Juni, 2024




*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701*

# OFISI ZA MATANGAZO

MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,

PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.

MOB: +255 - 0677020701

E-mail: advertise@guardian.co.tz,

Website: www.ippmedia.com

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Ruto atii sauti ya umma, akataa kusaini muswada

**NAIROBI,** Kenya

RAIS wa Kenya, William Ruto, amekataa kutia saini muswada wa fedha wa mwaka 2024, uliosababisha maandamano yaliyoambatana na vurugu kwenye taifa hilo.

Katika hotuba yake Ruto, amesema amesikia sauti ya Wakenya wengi waliopinga muswada huo na kwamba ameurejesha bungeni ili ufanyiwe marekebisho.

Amesema kwa kutosainiwa muswada huo na kuwa sheria, bajeti ya serikali itakuwa na pengo na kusababisha baadhi ya shughuli kusimama.


Rais Ruto, alisema katika namna ya kuziba pengo hilo kutakuwapo na mazungumzo ya kitaifa ili kuangalia nchi itakavyoendeshwa.

Hata hivyo, alieleza kwamba kuanzia sasa serikali yake itabana matumizi kwa kupunguza safari za nje katika ofisi yake, kusimamisha baadhi ya miradi ya ukarabati wa majengo na ununuzi wa magari mapya.

Alitaka mihimili mingine ikiwamo Bunge, Mahakama pamoja na taasisi zingine za serikali kuchukua hatua kama hiyo ili kupunguza matumizi.

Kwenye hotuba yake, Rais Ruto, ameweka wazi kwamba yuko tayari kukutana na vijana walioandamana maarufu kama Gen Z' kwa ajili ya kufanya nao mazungumzo kwa kushirikiana na viongozi wa dini.

Alifafanua kuwa atakutana na vijana hao kuanzia Jumapili wiki hii kwa lengo la kusikiliza madai yao.



Rais Ruto, alisema amesikitishwa na vifo vilivyotokea wakati wa maandamano hayo na kutoa pole kwa wazazi na ndugu waliofiwa, pamoja na kuwatakia kupona haraka waliojeruhiwa ambao wako hospitalini wakipatiwa matibabu.

Kabla ya kiongozi huyo kuzungumza na wananchi, Spika wa Bunge la Taifa, Moses Wetangula, amewasifu vijana kwa ujasiri wao ila alilaumu malalamiko yao hayakufuata mkondo wa sheria.

Maandamano hayo yaliyofanyika Jumanne ya wiki hii, yamesababisha watu 18 kuuawa na wengine zaidi ya 160 kujeruhiwa.

Viongozi wa vuguvugu hilo la maandamano lililopewa jina la 'Siku saba za hasira', kabla ya hotuba ya Rais Ruto, walisisitiza kuendelea na dhamira yao ya kuandamana leo.

Kupitia mtandao wa kijamii wa X, walisambaza ujumbe unaotumia hashtagi ya "Tukutane Alhamisi" ambao umesisitiza hawatarudi nyuma katika maandamano hadi hapo serikali itakapokubali matakwa yao.

Wakati huo huo, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Antonio Guterres, amevitaka vikosi vya polisi na usalama kujizuia na kutumia nguvu kupita kiasi huku akitoa wito wa kufanyika maandamano ya amani.

Zaidi ya mataifa 13 ya Ulaya yameelezea wasiwasi wao kufuatia ghasia zilizoshuhudiwa juzi na kusababisha polisi kuwaua watu hao kwa kuwapiga risasi.

Katika taarifa yao ya pamoja, balozi za nchi 13, zikiwamo Canada, Ujerumani, Uingereza na Marekani, zimetaja kushtushwa mno na matukio yaliyoshuhudiwa nje ya viwanja vya bunge.

Aidha, Mwenyekiti wa Halmashauri Kuu ya Umoja wa Afrika, Moussa Faki Mahamat, ameitaka nchi hiyo kuwa na utulivu na kujiepusha na ghasia zaidi.

Kwa upande wa Rais mstaafu wa Kenya, Uhuru Kenyatta, alisema amesikitishwa kwa maafa yaliyotokea nchini mwake wakati wa maandamano hayo na kuongeza kuwa ni haki ya kila Mkenya kuandamana kwa mujibu wa katiba.

Kiongozi huyo wa zamani aliwataka viongozi kusikiliza vilio vya wananchi.

Kiongozi wa upinzani nchini Kenya, Raila Odinga, alitoa wito wa kukomeshwa kwa vitendo vya ukatili dhidi ya waandamanaji na kushinikiza kufanyika kwa mazungumzo na kuitaka jumuiya ya kimataifa kuingilia kati.

***DW***

## Homa ya nyani yaleta hofu DRC

**KIVU, DRC**

AINA mpya ya virusi vya ugonjwa wa mpox, unaojulikana kama homa ya nyani, inayosambaa kwa kasi katika mpaka wa mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) umeanza kutia hofu.

Maofisa wa afya wanaofuatilia kuenea kwa ugonjwa huo, walisema aina hiyo mpya ya virusi vinasababisha mtu kupata vidonda mwili mzima na kuwafanya baadhi yao kuzidiwa na kuua.

Mlipuko wa sasa umechangiwa na maambukizi kupitia ngono lakini kuna ushahidi kwamba aina hii ya ugonjwa pia inaweza kuenezwa kupitia mgusano kimwili kati ya watu wawili au zaidi.

Wataalamu wa afya duniani walisema aina hiyo mpya ya virusi inaweza kuvuka mpaka na kuenea kimataifa.

Ugonjwa wa mpox ulidhibitiwa mnamo 2022 kwa kuwachanja watu walio hatarini kuambukizwa.

Hata hivyo, upatikanaji wa chanjo na matibabu nchini DRC umekuwa na changamoto.

Maofisa wa afya nchini humo walionya kwamba virusi hivyo vinaweza kufikia nchi zingine.

„Ugonjwa unaweza kupitia viwanja vya ndege. Mtu mwenye vidonda anaweza kupitia mipakani kwa sababu hakuna udhibiti," alisema Leandre Murhula Masirika, ofisa mkuu wa idara ya afya katika jimbo la Kivu Kusini, moja ya maeneo yaliyoathirika zaidi.

***BBC.***

# Vijana kushindanishwa kupata mtaji wa kilimo

**Na Romana Mallya**

SHIRIKA la Heifer International kwa kushirikiana na kampuni ya Sahara Vectures wameandaa shindano la kuwania ruzuku ya mtaji wa Sh. milioni 63.7 kwa vijana wa Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar wanaojishughulisha na kilimo.

Shindano hilo linalenga kuleta mapinduzi makubwa katika sekta ya kilimo. Mitaji itatolewa kupitiwa programu ya AYuTe Africa Challenge 2024 ambayo mshindi wa kwanza atajishindia Sh. milioni 28, wa pili Sh. milioni 21 na wa tatu Sh. milioni 14.

Akizungumza kuhusu shindano hilo jana jijini Dar es Salaam, Meneja wa Mradi wa AYuTe Africa Challenge Tanzania 2024, Emmanuel Senzighe, alisema moja ya vigezo vya shindano hilo ni kijana kusajili kampuni yake si chini ya miaka mitatu akiwa na kitu anachofanya.

"Faida ni kupata ruzuku za mitaji Sh. milioni 63.7 zitakazotolewa kwa washindi hao watatu pamoja na msaada wa mafunzo na ushauri wa kitaalamu namna ya kuboresha biashara zao na kuwaunganisha na fursa za kifedha na uwekezaji," alisema.

Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Heifer Tanzania, Mark Tsoxo, alisema kilimo kinahitaji nguvukazi kwa kuwa idadi ya watu na teknolojia na rasilimali zilizopo zina nafasi kubwa katika kuleta matokeo makubwa katika sekta hiyo.

"Tumekwenda kwa kundi la vijana kwa kuwa idadi yao ni wengi, hivyo tukiwapata wengi katika sekta ya kilimo tutaleta mapinduzi makubwa.

"Teknolojia ni muhimu katika sekta ya kilimo wakiwapo vijana kutakuwa na uhuhishaji wa teknolojia katika sekta hii na mabadiliko yatakuwa makubwa," alisema.

Pia alisema vijana wana maarifa na dunia inataka wafanye kazi kama kijiji na kundi hilo litaifanya nchi kuwa shindani katika sekta hiyo.

Alisema Heifer ni mfadhili wa programu hiyo na Sahara Ventures ni mtekelezaji, kwa kuwalenga vijana.

Kuhusu matarajio yao, Tsoxo alisema hadi mwaka 2030, shirika hilo linalenga kufikia wakulima 400,000 ambapo kati yao, 100,000 ni vijana wenye umri kati ya miaka 15 hadi 35.

Alifafanua kwamba katika mashindano huwafikia vijana kati ya watatu hadi watano na lengo ni kuendeleza vijana katika sekta ya kilimo.

"Tunatambua zama hizi zimekumbwa na mabadiliko mbalimbali ya tabianchi, ukame, vimbunga na mvua kubwa, hivyo kuathiri dhima yetu ni kuondoa njaa, kupunguza umaskini na kutunza mazingira," alisema.

Ofisa Mtendani Mkuu wa Kampuni ya Sahara Ventures, Jumanne Mtambalike, alisema wamekuwa wanasaidia mawazo ya vijana hususan kwenye ubunifu, teknolojia na ujasirimali ili kuwakwamua kiuchumi.

Alisema wao pamoja na Heifer International wameandaa programu hiyo kuangalia namna ya kuwasaidia vijana na mawazo waliyonayo katika sekta ya kilimo kwa kuwapatia ujuzi, mitaji na kuwaunganisha na watu watakaowasadia katika biashara zao kukua zaidi.

Alisema wanaangalia vijana wa kitanzania wanaofanya shughuli zao za kilimo kwa ubunifu na teknolojia kufikisha sokoni wanachozalisha na kutengeneza ajira.

Alisema zaidi ya asilimia 65 ya ajira zinazotoka Afrika zinatokea sekta ya kilimo ambayo inachangia zaidi ya asilimia 32 ya Pato la Taifa (GDP) barani Afrika.

# Coastal Union kusajili wazoefu

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Coastal Union imesema itasajili wachezaji wasiopungua watano ambao wote ni lazima wawe wamecheza michuano ya kimataifa inayosimamiwa na Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF).

Kiungo mshambuliaji, Mrundi Saido Ntibazonkiza, ambaye ameachwa na Simba na nyota wa zamani wa Yanga, Tuisila Kisinda, raia wa Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC), wanatajwa kuwa kwenye mawindo na timu hiyo.

Ofisa Habari wa timu hiyo, Abbas El Sabri, ameliambia gazeti hili mpaka sasa wanachelewa kutangaza majina ya wachezaji waliowasajili kutokana na mchakato wa kuwapata kutumia mrefu na mgumu.

Sabri aliweka wazi changamoto hiyo inatokana na wachezaji waliofanya nao mazungumzo ni wenye viwango vya juu na hadhi ya kimataifa.

"Tunataka kusajili wachezaji wasiopungua watano kuelekea msimu ujao, sifa ya kwanza ni lazima awe na uzoefu wa mechi za kimataifa, kwa maana ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho, ni lazima atoke katika klabu ambazo zimeshiriki michuano hiyo.

Tunataka huo uzoefu tuulete kwenye klabu yetu ya Coastal Union, hilo ndilo ambalo linatufanya mpaka sasa tuchelewe hata kuwatangaza, hasa ukizingatia mchakato wa kuwapata wachezaji wa aina hiyo ni mkubwa na migumu," Sabri alisema.

Aliongeza bado Coastal Union ina kikosi bora na ndiyo maana ilimaliza katika nafasi ya nne kwenye msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliomalizika, hivyo maingizo yanayotakiwa ni machache.

"Hatutaki tuingize watu wengi, kwa sababu tumeshaona tupo vizuri eneo gani na tuna udhaifu wapi, hivyo tutayafanyia kazi maeneo madogo tu, kwa sasa tunamalizana na wachezaji tutakaowasajili kifedha na wengine ni lazima tuvunje mikataba kwa klabu wanazozitumikia," aliongeza Sabri.

Timu nyingine itakayoshiriki mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika ni Simba huku mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga na Azam FC watapeperusha bendera ya nchi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

# AZAM FC : HATUJAMALIZA KUSAJILI WACHEZAJI WAPYA

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI ikiendelea kutangaza majina ya nyota inaowaacha, uongozi wa Azam FC umesema bado hawajamaliza kufanya usajili wa wachezaji kwa ajili ya msimu mpya wa mashindano, imefahamika.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Azam FC, Thabit Zacharia, amesema wakati wanaendelea kutangaza majina ya wachezaji ambao hawatakuwa sehemu ya mipango yao, mabosi wako katika hatua za mwisho za kusajili nyota wapya.

Zacharia alisema timu yao inafanya usajili kwa umakini na kwa sasa imewaacha vigogo wa soka waendelee na mchakato huo.

"Sio kama tumemaliza, bali tumeacha kelele za klabu nyingine zimalizike ili tuendelee kushusha wachezaji wengine wapya, tutaongeza wengine na bila shaka ndani ya klabu yetu wapo watakaoondoka, ndiyo maisha ya mpira yalivyo, mnaweza kuvamiwa na klabu yenye pesa mkashindwa kumzuia.

Kimsingi hatubomoi kikosi, ila tunakijenga, tutabaki na wachezaji wetu wote bora, tunaongeza wengine bora ili kuifanya timu iwe bora zaidi ili msimu ujao tuweze kufanya vyema zaidi," Zacharia alisema.

Tayari Azam imeachana na wachezaji watano mpaka sasa, wageni watatu na wazawa wawili mpaka sasa ni beki wa kati Mghana Daniel Amoah, kiungo mkabaji, Issa Ndala, ambaye ni Nigeria na Malickou Ndoye ambaye pia ni beki wa kati.

Mchezaji mwingine aliyetemwa ni beki wa kushoto, Edward Manyama na winga, Ayuob Lyanga ambao ni Watanzania.

Azam imetangaza itakwenda kuweka kambi yake Morocco na tayari imesajili wachezaji wapya watano, nyota wanne wakiwa ni wa kigeni na mmoja Mtanzania.

Wachezaji waliosajiliwa ni Jhonier Alfonso Blanco, akitokea klabu ya Rionegro Aguilas na kiungo mkabaji, Ever Meza, nyota wa zamani wa Leonnes FC, wote ni raia wa Colombia, beki wa kati, Yoro Mamadou Diaby aliyekuwa akiichezea Stade Malien de Bamako ya Mali pamoja na kiungo mshambuliaji kutoka timu hiyo hiyo, Franck Tiesse, wote wakiwa ni raia wa Mali.

Straika Adam Adam kutoka Mashujaa FC ya Kigoma naye amemwaga saini ndani ya timu hiyo ambayo itashiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.




Wachezaji wa soka wa umri chini ya miaka 15 (U-15), wakifanya mazoezi katika Kituo kinachosimamiwa na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF) kilichoko Mnyanjani jijini, Tanga jana. **PICHA: TFF**

# UCHAGUZI WANAWAKE MARA JULAI

**Na Mwandishi Wetu**

CHAMA cha Mpira wa Soka la Wanawake Mkoa wa Mara (FWAM), kinatarajia kufanya uchaguzi Mkuu Julai 14, mwaka huu imeelezwa.

Mwenyekiti wa Kamati ya Uchaguzi ya Chama Cha Mpira wa Miguu Mkoa wa Mara (FAM), Stamili Ndaro, aliliambia gazeti hili nafasi zinazowaniwa katika uchaguzi huo ni ya Mwenyekiti, Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Taifa na Wajumbe wawili wa Kamati ya Utendaji.

Ndaro alisema ada ya kuchukua fomu kwa watakaogombea uenyekiti ni Sh. 100,000 na Sh. 70,000 kwa watakaotaka nafasi ya Ujumbe wa Mkutano Mkuu Taifa na nafasi iliyobakia ni Sh. 50,000.

**Alisema usaili wa wagombea utafanyika Juni 30, mwaka huu na orodha ya mwisho ya wagombea watakaokuwa wamepitishwa kuwania nafasi hizo za uongozi itatatangaza Julai 8, mwaka huu.**

"Kampeni zitafunguliwa rasmi kuanzia Julai 10, mwaka huu, tunaamini wagombea watafuata kanuni na taratibu ili kujiweka katika nafasi salama," Ndaro alisema.

Mikoa 20 ya Tanzania Bara tayari imeshafanya uchaguzi wake kwa ajili ya kuelekea katika uchaguzi wa Chama cha Mpira wa Miguu cha Taifa (TWFA), ambao utafanyika baadaye mwaka huu.

## ZISIKUPITE

### EZE ATAKIWA SPURS
KLABU ya Tottenham Hotspur inavutiwa na mshambuliaji wa Crystal Palace na Timu ya Taifa ya England, Eberechi Eze, mwenye umri wa miaka 25, na wanaweza kutafuta kuamsha kipengele cha kumwachia katika mkataba wake. (Talksport)

### HALL ANUKIA BRIGHTON
KLABU ya Brighton inamtaka kiungo wa kati wa Leicester, Kiernan Dewsbury-Hall, mwenye umri wa miaka 25. (Telegraph)

### BAKAYOKO ATAJWA ARSENAL
ARSENAL wameuliza kuhusu kumsajili mshambuliaji wa PSV Eindhoven, ambaye ni raia wa Ubelgiji, Johan Bakayoko. (DHNet)

### FEENEY AKARIBIA SPURS
TOTTENHAM Hotspur imezishinda timu kadhaa za Ligi Kuu England katika mchakato wa kumsajili mshambuliaji wa Glentoran mwenye umri wa miaka 16, George Feeney, ambaye amewakilisha Ireland Kaskazini na Wales katika ngazi ya vijana. ***(Football. London)***

### SANCHO KUTUA BARCA
BARCELONA inavutiwa na mkataba wa mkopo wa winga, Jadon Sancho, mwenye umri wa miaka 24, baada ya kufanya mazungumzo na Manchester United. ***(Sport)***

### BAYERN NJIA PANDA
KLABU ya Bayern Munich bado inavutiwa na kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Ureno, Joao Palhinha, mwenye umri wa miaka 28, lakini wanapungukiwa sana na dau la pauni milioni 60 lililotakiwa na Fulham. ***(Telegraph)***

### VILLA YAMTAKA GONCALVES
KLABU ya Aston Villa inafikiria kumnunua winga wa Sporting Lisbon, Pedro Goncalves, mwenye umri wa miaka 25. ***(A Bola)***

### JOHNSON ANAENDA IPSWICH
KLABU ya Ipswich ipo katika mazungumzo na beki wa England, Ben Johnson, mwenye umri wa miaka 24 kuhusu uhamisho wa bila malipo ya mkataba wake wa West Ham utakapokamilika wiki ijayo. ***(East Anglian Daily Times)***

### RABIOT KUTUA UNITED
MANCHESTER United imefanya mazungumzo na Juventus kuhusu kumsajili Adrien Rabiot, lakini wanakabiliwa na ushindani kutoka kwa Arsenal na Aston Villa katika kumnunua kiungo huyo Mfaransa mwenye umri wa miaka 29. ***(TeamTalks)***

### KINDA BAIDOO SOKONI
KLABU ya Nottingham Forest na Brighton inavutiwa na winga wa Norway na klabu ya Sogndal, mwenye umri wa miaka 18, Edmund Baidoo. ***(Sky Sports)***,

### TEN HAG KIMEELEWEKA
KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag, anatarajiwa kusaini mkataba mpya kwa ajili ya kuendelea kuiongoza timu hiyo kuelekea msimu mpya wa mashindano. ***(Fabrizio Romano)***

### ROCA, LEEDS KUTETA
KIUNGO wa kati wa Leeds United, Marc Roca, mwenye umri wa miaka 27, yuko katika hatua za mwisho za mazungumzo na Real Betis kuhusu kusaini mkataba wa kudumu baada ya kusajiliwa na klabu hiyo kwa mkopo msimu uliopita. ***(Football Insider).***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# SOUTHGATE: NAUMIA ENGLAND KUZOMEWA

**Kocha huyo awataka mashabiki kuendelea kuipa sapoti timu...**

**COLOGNE,** UJERUMANI

GARETH Southgate amehoji "mazingira yasiyo ya kawaida" yanayoizunguka England baada ya kuzomewa dhidi ya Slovenia licha ya kuongoza katika Kundi C na kuwataka wafuasi kuiunga mkono timu hiyo.

England walipiga mashuti manne pekee yaliyolenga lango katika matokeo mengine duni kwenye michuano ya Mataifa ya Ulaya.

Wakati Southgate alipoenda kwa mashabiki wa England baada ya kumalizika kwa mchezo huo, baadhi waliitikia vyema lakini wengine walizomea.

Mkataba wa sasa wa Southgate na Chama cha Soka cha England utamalizika Desemba na uamuzi utachukuliwa kuhusu mustakabali wake baada ya fainali hizo.

Baadhi ya mashabiki wamehoji kama yeye bado ni mtu sahihi kuinoa England baada ya kuiongoza kwa miaka nane na Southgate alisema kuhusu majibu ya muda wote: "Ninaelewa. Sitarudi nyuma. Jambo muhimu zaidi hapa ni wafuasi wabaki na timu.

„Ninaelewa simulizi kwangu na hiyo ni bora. Lakini inaunda mazingira yasiyo ya kawaida ya kufanya kazi.

"Ninatambua unapokuwa na wakati wa mwisho wa mchezo, ninawaomba wachezaji wasiwe na woga, sitarudi nyuma na kuwashukuru mashabiki ambao walikuwa wazuri wakati wa mchezo.

"Wanaweza kuhisi tofauti kwangu. Lakini kwangu, tutafaulu tu ikiwa tutakuwa pamoja. Nguvu hiyo ni muhimu kwa timu na ni muhimu sana kubaki na timu."

Alipoulizwa ni nini kimebadilika kuhusu mazingira yanayoizunguka timu, Southgate alijibu: „Nadhani pengine matarajio. Tumeifanya England kwa miaka sita au saba iliyopita ya kufurahisha tena. Nadhani imekuwa ya kufurahisha kwa wachezaji. Inabidi kuwa makini sana, sana inabaki hivyo."

Licha ya majibu kutoka kwa baadhi ya mashabiki, nahodha wa timu ya taifa ya England, Harry Kane, alisema anafikiri kulikuwa na kiwango kizuri zaidi kutokana na mchezo wa awali wa timu hiyo ilipotoka sare ya 1-1 na Denmark.

"Hilo ndilo lilikuwa lengo kabla ya kuanza kwa mashindano, njoo juu ya kundi na udhibiti hatima yetu," aliiambia ITV. „Nilidhani tulicheza vizuri zaidi kuliko michezo mingine. Hatukupata tu mwisho huo lakini tunatazamia mwingine."

„Tulitengeneza nafasi za nusu na kulikuwa na ambazo labda tungefanya vizuri zaidi."

# ARGENTINA YATINGA ROBO FAINALI YA COPA AMERICA

**ATLANTA,** MAREKANI

MABINGWA watetezi wa Kombe la Mataifa ya Amerika Kusini, Argentina imekuwa timu ya kwanza kutinga hatua ya robo fainali ya michuano hiyo inayofanyika Marekani baada ya kuifunga Chile bao 1-0 hapo juzi.

Argentina inaongoza Kundi A ikiwa na pointi sita baada ya kushinda mechi mbili, ikifuatiwa na Canada yenye pointi tatu, Chile ina pointi moja sawa na Peru inayoburuza mkia.

Bao la Argentina lilifungwa na Lautaro Martinez katika dakika 88 ya mchezo baada ya nahodha, Lionel Messi kuchonga kona iliyosababisha piga nikupige langoni mwa Chile.

Mchezo wa mwisho wa Argentina wa makundi utachezwa keshokutwa dhidi ya Peru.

## Nacho aondoka Madrid baada ya kukaa miaka 23

**MADRID,** HISPANIA

KLABU ya Real Madrid imethibitisha kuondoka kwa nahodha wao, Nacho Fernandez, baada ya miaka 23 akiwa hapo.

Madrid imechapisha taarifa katika mitandao yake ya kijamii ikimshukuru Nacho kwa miaka mingi aliyohudumu klabuni hapo na kuwa mmoja ya wachezaji wa kutegemewa waliopata mafanikio makubwa timu yao.

Nacho naye ameandika katika kurasa zake za mitandao ya kijamii akishukuru klabu hiyo.

Nacho alijiunga na klabu hiyo mwaka 2001 na alifanikiwa kuichezea mechi ya kwanza kwenye kikosi cha wakubwa mwaka uliofuata.

Katika kipindi hicho, ameichezea Real Madrid michezo 364, akibeba mataji 26 na hivyo kumfanya kuwa mchezaji mwenye mataji mengi zaidi klabuni hapo, sambamba na Luka Modric.

Nacho amefanikiwa kuisaidia Madrid kutwaa taji la 15 la Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa kama nahodha na ubingwa huo umemfanya kuwa na mataji sita, mataji mengi zaidi kuliko mchezaji mwingine yeyote akiungana na Modric, Toni Kroos, Dani Carvajalna Francisco Gento.




## Deschamps: Maski 'inamkera' Mbappe

**DORTMUND,** UJERUMANI

KOCHA wa Ufaransa, Didier Deschamps, aliangazia matatizo ambayo, Kylian Mbappé, alikumbana nayo akiwa amevalia maski ili kulinda pua yake iliyovunjika katika sare ya 1-1 dhidi ya Poland kwenye michuano ya Ulaya iliyochezwa juzi.

Mbappé alifunga penalti kipindi cha pili kuashiria kurejea kwake katika kikosi cha kwanza cha Ufaransa, siku nane baada ya kupata jeraha la damu mwishoni mwa ushindi wa 1-0 dhidi ya Austria hapo Juni 17, mwaka huu.

Deschamps alisema kabla ya mchezo maoni ya pembeni ya Mbappé yatakuwa na kikomo kwa sababu ya maski hiyo, lakini kulikuwa na suala jingine la joto kali huko Dortmund.

„Licha ya yote aliyopitia, wiki moja baada ya kipigo hicho, ilikuwa ngumu," Deschamps aliwaambia waandishi wa habari.

„Nilidhani alikuwa mzuri sana kwa miguu yake na maski. Alihitaji kuizoea.

„Lakini wakati anatokwa na jasho, hiyo inashikamana na macho yake na alihitaji kufuta macho yake."

Bado, Deschamps alifurahishwa na uchezaji wa Mbappé, baada ya kumwacha mshambuliaji huyo anayekwenda Real Madrid.

„Ana njaa ya kucheza na mchezo ungemsaidia vizuri," aliongeza Deschamps.

Bao la Mbappe halikutosha kwa ushindi na halikutosha kutatua matatizo yaliyokuwa kwa Ufaransa katika michuano hiyo ya Euro 2024.

Mbappé aliondoa maski yake ili kusherehekea mbele ya mashabiki wa timu yake baada ya kufunga penalti dakika ya 56.

Lakini Robert Lewandowski aliihakikishia Poland sare ya 1-1 kwa penalti dakika ya 79, na kuwaacha Wafaransa wakiwa washindi wa pili wa Kundi D nyuma ya Austria.

## HABARI MICHEZO

# MASHABIKI SIMBA SC, YANGA WAFUNGUKA NGUVU YA CHAMA

**Na Somoe Ng'itu**

WAKATI bado haijawekwa hadharani, Clatous Chama, ataitumikia klabu ipi katika msimu ujao wa mashindano, mashabiki wa Simba na Yanga kutoka sehemu mbalimbali nchini, wametoa maoni yao kuhusiana na kiungo huyo raia wa Zambia.

Chama amebakiza siku tatu tu katika mkataba wake na Wekundu wa Msimbazi.

Akizungumza jijini jana, shabiki wa Yanga, Azizi Kalinga, alisema kiungo huyo ni mmoja wa wachezaji wenye uwezo mkubwa kwa sasa na hakuna timu ambayo ikifanikiwa kumpata itajutia usajili huo.

Kalinga alisema mchezaji huyo ana uzoefu na amekuwa akisaidia timu yake kupata matokeo muhimu na hiyo inatokana na kipaji alichonacho.

"Sisi tumejipanga na tumekamilika, tuna uwezo wa kumpata mchezaji yoyote tunayemhitaji hapa Tanzania, hatutamkosa, iwe Clatous Chama au Prince Dube, hatuwezi kushindwa kumsajili ," alisema shabiki huyo.

Amri Diaz, alisema anaamini walifanikiwa kumnasa Chama, kikosi chao kitakuwa imara na kitatoa ,dozi' kwa kila watakayekutana naye.

"Naona kabisa kuna mtu atakula 10 msimu ujao, huku Chama huku Dube, tutakuwa na kikosi tishio Afrika, tunaamini hakuna atakayeweza kututisha, hakuna atakayeingia mguu wake akatoka salama," alitamba shabiki huyo wa Yanga.

Aliongeza lengo la Yanga kusajili wachezaji mbalimbali ambao ni mahiri na wazoefu ni kutaka kuhakikisha wanafikia malengo yao ya kufanya vyema kwenye mashindano ya kimataifa yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Naye mwanachama wa Simba, Fadhila Juma, alisema bado Chama ni mchezaji muhimu ambaye anahitajika ndani ya kikosi chao.

Alisema kumwacha Chama kwa sasa hautakuwa uamuzi wa busara kwa sababu timu yao inahitaji kuimarishwa katika idara zenye mapungufu.

"Kumwacha Chama si uamuzi mzuri, kwa upande wangu naona bado ana nafasi na mchango mkubwa katika kikosi chetu, kwa sasa unaweza kuleta mtu mpya, je kama atashindwa kuonyesha uwezo wake au kuingia katika mfumo itakuaje, itaigharimu timu," alisema shabiki huyo.



Washiriki wa Kozi ya CAF B Diploma (waliosimama), wakimsikiliza Mkufunzi kutoka Shirikisho la Soka Afrika (CAF) katika mafunzo yanayoendelea jijini Tanga. **PICHA: TFF**

# Malindi yaacha wachezaji 14

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

BAADA ya kufanya vibaya katika msimu uliomalizika, uongozi wa Malindi SC umesema hawataki kurudia makosa na wamejipanga kukamilisha mapema mchakato wa usajili.

Malindi ilimaliza katika nafasi ya 10 ikiwa na pointi 36 katika msimu uliomalizika wa 2023/2024, wakishinda michezo 10, sare ya sita na imefungwa michezo 14.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa Malindi, Suleiman Mohamed 'Kocha Mo' alisema wameanza na uamuzi wa kuwaacha wachezaji 14 ambao walikuwa katika kikosi cha msimu uliomalizika.

Kocha huyo alisema wanajipanga kufanya usajili ,mkubwa' ambao utawapa matokeo chanya na hatimaye kurejesha makali yao katika Ligi Kuu Zanzibar msimu ujao.

"Tunafanya maboresho mapema katika kikosi chetu, tumeona hatukuwa na msimu mzuri, hatukuwa bora sana, tulibakia kupambana ili kuibakisha timu Ligi Kuu, msimu ujao tunataka turejee kivingine," alisema kocha huyo.

Hata hivyo aliongeza msimu uliopita ligi ilikuwa na ushindani na hakukuwa na mechi rahisi na hiyo imesaidia kuchelewa kupatikana kwa bingwa na timu zilizoshuka daraja.

"Tulikosa washambuliaji wazuri, eneo hili lilikuwa ndio changamoto zaidi katika upande wetu, sasa tunalitupia macho kwa ukubwa katika kusaka wachezaji wenye uwezo," aliongeza.

# Simba yampa Chama masharti

INATOKA UK. 24

Mbali na Mzamiru, Simba pia imetangaza kumwongezea mkataba beki Israel Patrick, Kibu Denis na Shomari Kapombe kuendelea kuitumikia timu hiyo kwa ajili ya msimu ujao wa Ligi Kuu na michuano ya Kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Katika hatua nyingine, kiungo mshambuliaji raia wa Zambia, Joshua Mutale ambaye inaelezwa amesaini mkataba wa miaka mitatu kuitumikia timu hiyo, amewasili nchini juzi usiku.

Kiungo huyo aliyekuwa akiichezea klabu ya Power Dynamos ya nchini humo, msimu ujao atavaa jezi nyekundu kuitumikia timu hiyo ya Msimbazi.

## Serikali yazitaka Yanga, Simba kufanya usajili mzuri kimataifa

INATOKA UK. 24

Alisema ana uhakika timu zote, hata Azam na Coastal Union ambazo nazo zitacheza michuano ya kimataifa zitafanya vyema kwa sababu ligi ya Tanzania kwa sasa ni nzuri, hivyo timu zote zilizofuzu ziende kuleta ushindani mkubwa.

"Timu ziendelee kupeperusha bendera ya nchi na kama kawaida bao la mama litakuwapo kuanzia hatua kama ya msimu uliopita, kilichobaki wafanye usajili mzuri, waziandae timu vizuri, serikali iko nyuma ya timu zote," alisema Msigwa.

Aidha, alisema serikali itafunga kifaa cha kuwasaidia waamuzi (VAR) kwenye viwanja vipya itakavyojenga, Arusha na Dodoma.

"Tumefanya tathmini ya kutumia video ya kuwasaidia waamuzi VAR, Uwanja wa Benjamin Mkapa una uwezo wa kufungwa, viwanja vipya vya kisasa vitakavyojengwa Arusha na Dodoma navyo tutafunga vifaa hivyo, lakini wakati tunavikarabati viwanja vyetu vilivyopo sasa tutazingatia kuweka maeneo ya kufungwa miundombinu hiyo, hilo halina wasiwasi na serikali imeshaondoa kodi ya vifaa hivyo," alisema Msigwa.

Michezo
Nipashe Alhamisi Juni 27, 2024

## Southgate: Naumia England kuzomewa



UKURASA 21




# SIMBA YAMPA CHAMA MASHARTI

●●●Uongozi umemtaka kukubali masharti yao ili kumpa mkataba mwingine, vinginevyo ni...

**Na Faustine Feliciane**

WAKATI bado kukiwa na 'kizungumkuti' juu ya hatima ya mchezaji Clatous Chama kuhusu usajili wake, inaelezwa nyota huyo anayemaliza mkataba wake siku chache zijazo amepewa masharti na klabu hiyo ili waweze kumwongezea mkataba.

Awali kulikuwa na taarifa kuwa nyota huyo tayari amemalizana na viongozi wake na uwenda akasaini mkataba mpya huku pia Yanga wakihusishwa kumtaka, uongozi wa Simba umeamua kumbananisha Chama na kumtaka kukubali masharti yao ikiwamo dau walilomwandalia ili wampe mkataba mpya.

Taarifa kutoka ndani ya klabu hiyo zinasema kama mchezaji huyo hatakubali masharti hayo, uongozi umempa uhuru wa kuondoka.

"Kiukweli Chama bado hajasaini na mkataba wake nadhani umebaki siku chache sana, kulikuwa na mvutano ndani ya uongozi kuamua kama apewe mkataba mpya au waachane naye, sasa wamempa masharti ambayo kama atakubaliana nayo msimu ujao ataendelea kuichezea Simba, lakini bado hajasaini mkataba mpya, mashabiki wajiandae wanaweza wasimwone kwenye timu msimu ujao," kilisema chanzo chetu ndani ya klabu hiyo bila kutaja kwa ndani masharti hayo.

Aidha, alisema uongozi unakijenga upya kikosi cha timu hiyo ili kurejesha makali yao lakini wanataka kubaki na wachezaji watakaojitoa kwa ajili ya timu na hawatakuwa na usumbufu muda wote.

"Moja ya mambo yanayotajwa kutuangusha msimu ulioisha ni wachezaji kutojituma, hawajitoi kweli kwa ajili ya timu, sasa tunataka wachezaji watakaoipigania kweli jezi ya Simba, ndio maana unaona mchezaji kama Mzamiru (Yassin) ameongezewa mkataba kwa sababu ni mmoja wa wachezaji waliokuwa wakijituma," kilisema chanzo hicho.

INAENDELEA UK. 23



Mshambuliaji wa England, Phil Foden (kushoto), akiwania mpira na beki wa Denmark wakati wa mchezo wao wa Kundi C, Fainali za Euro 2024 juzi usiku, timu hizo zilifungana bao 1-1. **PICHA: MTANDAO**

# Serikali yazitaka Yanga, Simba kufanya usajili mzuri kimataifa

**Na Adam Fungamwango**

SERIKALI imezitaka klabu zitakazoiwakilisha nchi kwenye mashindano ya kimataifa zikiwamo Yanga na Simba kufanya usajili mzuri, makini na wa kiufundi, ili kufanya vyema kwenye michuano hiyo.

Mbali na klabu hizo, pia Azam FC na Coastal Union nao watashiriki michuano hiyo ya kimataifa ambapo Yanga na Azam zitashiriki Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba na Coastal Union zenyewe zitashiriki Kombe la Shirikisho Afrika.

Akizungumza jijini Dar es Salaam juzi jioni, Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Gerson Msigwa, alisema kufanya vizuri kwa timu hizo kwenye michuano hiyo ya kimataifa kutatokana na usajili wenye tija watakaofanya.

"Mimi nikizungumza kwa niaba ya serikali nazitaka Simba na Yanga zijiandae vizuri tunazitakia kila la heri, lakini zifanye usajili mzuri ili ziende kuiwakilisha vyema nchi, zifike hatua kama za msimu uliopita au zaidi, tunaendelea kufanya kazi kwa ukaribu na Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF) kuhakikisha kwamba ushiriki wetu unakuwa wa kimkakati na siyo kusindikiza watu wakatufunge," alisema Msigwa.

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >